SUPA JACKPOT
TZS. 1,139,859,317
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Unga** wa mtama suluhisho unene mkubwa, kisukari

UKURASA 3




UKURASA 9

Nipashe
JUMAPILI
MWANGA WA JAMII
Jumapili Agosti 6, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
www.ippmedia.com
ISSN 0856 • No. 0581394
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US

# ACT yaibua hoja tatu kupanda bei ya mafuta

• **LATRA** yaonya kupanda nauli, waagizaji wataja vikwazo... *Ukurasa 2&4*



Wanafamilia wakiwa na huzuni baada ya kuuaga mwili wa mpendwa wao, marehemu Neech Msuya, wakati wa ibada ya kumuaga iliyofanyika jana katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Kijitonyama, Dar es Salaam, kabla kusafirishwa kwenda Mwanga, Kilimanjaro kwa mazishi. Picha ndogo: Baadhi ya ndugu wakilia kwa uchungu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Vilio, simanzi vyatanda wazazi wakipita kuaga mwili bosi ABSA

UKURASA 3



## Mfumo sheria wa kudhibiti ushoga waiva

UKURASA 2

MICHEZO NZEGELI, KONKONI WATAJWA YANGA UK.24
KATUNI UK.6

# Mfumo Sheria wa kudhibiti ushoga waiva

**Na Thobias Mwanakatwe,**
MBEYA

TUME ya Kurekebisha Sheria Tanzania (LRCT) imesema iko katika hatua za mwisho za kukamilisha taarifa kuhusu Mfumo wa Sheria Unaosimamia Makosa dhidi ya Maadili Tanzania likiwamo suala la ushoga na ubakaji ili kutoa mapendekezo ya namna bora itavyoshughulikia makosa hayo kisheria.

Wakili wa Serikali kutoka katika tume hiyo, Ismail Hatibu, alimweleza hayo jana Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, alipotembelea banda la LRCT kwenye maonyesho ya wakulima na wafugaji (Nanenane) yanayofanyika kwenye viwanja vya John Mwakangale, jijini hapa.

Mbali na ushoga na ubakaji, Hatibu alisema taarifa hiyo inalenga kutoa mapendekezo yake kuhusu suala la madangulo, ulawiti na unyanyasaji wa kijinsia.

Alisema kutokana na maoni ya wananchi, matukio hayo yanaendelea kwa kasi nchini kwa sababu makosa hayo pamoja na mambo mengine humpa mtuhumiwa nafasi ya kupata dhamana, hali inayosababisha kuongezeka kwa kasi.

Hatibu alisema pia tume imekuwa ikitoa elimu ya sheria kwa umma ili kuwawezesha wananchi kutambua haki na wajibu wao.

Alisema kwa sasa tume imeshatoa ripoti 52 zinazotoa mapendekezo kuhusu marekebisho ya sheria mbalimbali. Mapendekezo hayo, alisema yameshirikisha maoni ya wananchi, mfano utungwaji wa Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 imezingatia maoni ya taarifa ya tume. "Ili tuendelee tunahitaji kuwa na sheria bora kwa maendeleo ya taifa, hivyo kwa kuzingatia hilo hadi sasa tume inaendelea kutoa elimu ya sheria kwa umma katika kanda mbalimbali," alisema.

Mtaka aliitaka tume kuwa karibu na wananchi ili waweze kutoa maoni mbalimbali kwa kuwa maendeleo ya nchi hutegemea msingi wa sheria zilizo bora na namna zinavyoweza kuwasaidia Watanzania.

Alisema tume inapaswa kuongeza wigo wa kujitangaza kupitia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii pamoja na kukutana na wananchi mara kwa mara ili kutoa elimu ya sheria mbalimbali ambazo zimebadilishwa.

Akizungumzia sheria ya ndoa, Mtaka alisema baadhi ya vijana wamekuwa wakikosa fursa za kuendelea na masomo kwa sababu ya kuolewa wakiwa na umri mdogo suala ambalo linakosesha maendeleo ya vijana na taifa kwa ujumla.



Mkuu wa wilaya ya Singida, Mhandisi Paskas Mulagiri (kushoto), akishiriki zoezi la kuchoma nyavu zisizo na viwango zilizokamatwa kutoka kwa wavuvi waliokuwa wakizitumia kuvulia samaki kwenye maziwa ya Kindai na Singidani katika Manispaa ya Singida mwishoni mwa wiki. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# ACT yaibua hoja tatu kupanda mafuta

**Na Waandishi Wetu**

CHAMA cha ACT Wazalendo kimependekeza kuchukuliwa hatua tatu kukabiliana na kupanda kwa bei za mafuta ya petroli na dizeli ili kumwondolea Mtanzania ugumu wa maisha.

Mwezi huu, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilitangaza bei mpya za mafuta na kuonyesha bei za rejareja za petroli zimeongezeka kwa Sh. 463 (sawa na asilimia 16.9) kutoka Sh. 2,736 za Julai hadi Sh. 3,199.

Bei ya dizeli imeongezeka kwa Sh. 391 (sawa na asilimia 15.3) kutoka 2,544 mwezi Julai hadi kufikia Sh. 2,935 mwezi huu kwa Dar es Salaam.

Kutokana na mabadiliko hayo, taarifa ya ACT Wazalendo iliyotolewa jana na Ofisi ya Wasemaji wa Kisekta, ilisema ongezeko hilo limezua taharuki na manung'uniko miongoni mwa wananchi na kusababisha gharama na mfumuko wa bei.

"Kumekuwa na malalamiko ya uhaba wa mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa katika maeneo mbalimbali nchini kama vile Kagera, Katavi, Manyara na baadhi ya maeneo mkoani Lindi.

EWURA ilitoka hadharani na kusema kwamba ni njama za baadhi ya wafanyabiashara kuficha bidhaa hiyo ili kusubiri bei ipande waingize sokoni.

"Tunaona ni muhimu sasa EWURA ijitafakari upya kuhusu utekelezaji wa mamlaka yake ili wananchi wa maeneo husika wasiendelee kupata tabu ya uholela wa kupanda bei na kukosa huduma," ilisema taarifa hiyo.

Chama hicho kilisema kupanda kwa gharama za bei ya mafuta kumetokana na serikali kuondoa ruzuku kwenye mafuta ya petroli na dizeli, kuongeza ushuru wa Sh. 100 kwenye kila lita na kuporomoka kwa thamani ya shilingi dhidi ya Dola ya Marekani kwa sababu ya uhaba wa dola.

Katika taarifa hiyo, ACT Wazalendo ilisema katika uchambuzi wa bajeti ya serikali kwa mwaka 2023/24, ilitaka serikali kuchukua hatua za haraka katika kupunguza matumizi ya fedha kuagiza bidhaa na huduma nje ya nchi.

Chama hicho kimezitaja hatua hizo, moja, ni kupunguza uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi.

"Serikali ianze kutekeleza matumizi ya nishati mbadala (gesi asilia). Kwa kuanzia magari yote ya serikali yaanze kutumia gesi asilia (CNG) ili kupunguza kutumia fedha nyingi za kigeni kuagiza bidhaa za mafuta.

"Pendekezo hili pia litasaidia kupunguza matumizi ya serikali kwa takribani Sh. bilioni 500 kwa mwaka. Hivyo basi, bohari zote za serikali (GPSA) zifungwe mitambo ya kujazia gesi asilia (CNG) mara moja," kimetaka.

ACT Wazalendo imeiomba serikali kuweka msisitizo kwenye utekelezaji wa mradi wa Mchuchuma na Liganga ili kuzalisha bidhaa za chuma kwa matumizi ya ndani na nje.

"Hii itasaidia kuokoa fedha za kigeni zaidi ya Dola za kimarekani bilioni 1.1 ambazo tunatumia kuagiza chuma kutoka nje kwa mujibu wa taarifa za serikali," imesema na kuongeza kuwa serikali iharakishe mradi wa kusindika Gesi Asilia wa Lindi (LNG) na kuufungamanisha na mradi wa kuanzisha kiwanda kikubwa cha kuzalisha mbolea.

Hatua hiyo, imesema itasaidia kuokoa fedha za kigeni zinazotumia kuagiza mbolea kutoka nje, ambapo mwaka 2022 ilitumia Dola milioni 503.

Hatua ya pili, kwa mujibu wa chamah icho, ni mahususi za kikodi kwa kuitaka serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kujenga hifadhi ya kutosha kutunza mafuta angalau ya kutosha miezi sita, ili kama kutatokea mabadiliko ya bei katika soko la dunia, yasiathiri uchumi kwa haraka.

"Serikali irejeshe utaratibu wa kutoa ruzuku ya mafuta kwa petroli na dizeli hadi hatua zingine za kukabiliana na bei zikamilike na tunarudia wito wetu iweke ruzuku ya Sh. 500.

Pia iondoe tozo ya Sh. 100 iliyoanzishwa katika mwaka wa fedha 2023/24," imesema.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, hatua ya tatu ni za kuongeza uzalishaji na mauzo nje ambapo chama hicho kimeitaka serikali mauzo ya bidhaa za kilimo nje yaongezwe ikiwamo kuongeza thamani ya mazao.

"Kwa mfano, korosho iliyobanguliwa inaweza kutuletea mpaka Dola milioni 500 kwa mwaka na soya (kwa kuuza China) inaweza kuingiza mpaka Dola bilioni moja. Vivyo hivyo, kwa mazao kama ya ufuta, mbaazi, kahawa na pamba yanaweza kutuletea fedha nyingi zaidi za kigeni kwa kuongeza tija na uzalishaji," ilisema.

Pia ilishauri kuweka vivutio katika sekta ya utalii kwa kuongeza matangazo na kuboresha miundombinu ya utalii ili kuongeza idadi ya watalii maradufu ya idadi ya sasa.

Chama hicho kilisema endapo nchi ikifikisha watalii milioni tano kwa mwaka, itapata fedha za kigeni mara tatu ya inazopata sasa na kuongeza ajira nyingi kwa watanzania.

Kadhalika kuongeza ufanisi katika bandari ili kufaidika na uchumi wa jiografia kwa kuongeza idadi ya mizigo inayopita na kutoka nchi jirani maradufu ya inayohudumia sasa.

"Sasa hivi mapato ya fedha za kigeni tunayoyapata kwa huduma za usafirishaji (transit trade) ni takribani Dola bilioni 1.9 tu kwa mwaka 2022, ilihali uwezo wetu ni wa kufikia mpaka Dola bilioni 12 kwa mwaka," kimesema.

Katika taarifa hiyo, ACT Wazalendo ilisema changamoto ya uhaba wa fedha una mchango mkubwa kwenye kuongeza bei za bidhaa na huduma zinazonunuliwa kutoka nje.

**WANANCHI, LATRA**

Baadhi ya abiria mkoani Katavi wakizungumza na mwandishi wa habari hizi walisema kwa sasa nauli ya kutoka Mpanda-Kijiji cha Uruwila ikiwa ni umbali wa takribani kilometa 30 kutoka mjini ni Sh. 4,000 badala ya Sh. 2,000 ya awali.

"Tunaomba serikali iliangalie hili. Tumezoea mafuta yakipanda bei za nauli haizidi 200 lakini sasa bei inapanda mara nne ya ongezeko la bei za upandaji wa mafuta,"alisema Joseph James.

"Awali tuliambiwa nauli imepanda kwa sababu ya mafuta hayapatikani na sasa yanapatikana wanasema bei kununua ipo juu. Dereva mmoja leo (jana) kipindi tunakuja tumeshuhudia akipigwa na abiria sababu ni kupandisha nauli," alisema Kalenga Sadiki.

Dereva Moshi Hussein alisema kwa sasa wananunua mafuta Sh. 3,357 kwa lita na wanalazimika kuongeza nauli ili kufikia gharama kwa sababu safari kutoka Mpanda-Uruwila ni kilometa 40 na hutumia lita 12 kwenda na kurudi.

Ofisa Mfawidhi kutoka LATRA mkoani hapa, Aleni Mwanry, alisema mamlaka haijatangaza kupanda kwa bei za nauli na kusisisitiza kwamba, mchakato wa upandishaji hushirikisha wadau kwa kupeleka mapendekezo.

Mwanry alikiri kuwapo kwa ongezeko la nauli huku akiwaonya wasafirishaji kuwa atakayeiongeza wakati mamlaka haijatangaza nauli mpya, atachukuliwa hatua.

**Imeandaliwa na Romana Mallya (DAR) na Neema Hussein (KATAVI).**

# Unga wa mtama suluhisho kiafya wenye unene uliopitiliza, kisukari

**Na Ashton Balaigwa,** MBEYA

MTAFITI Mwandamizi Usindikaji na Uongezaji Thamani kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Ukiriguru mkoani Mwanza, Dk. Caresma Chuwa, amesema unga wa mtama una faida ambazo zinaweza kuwa suluhisho kwa wenye uzito mkubwa uliopitiliza.

Katika maonyesho ya kimataifa ya wakulima, wafugaji na wavuvi yanayofanyika kitaifa katika Viwanja vya John Mwakangale jijini hapa, mtaalamu huyo alisema suluhisho hilo linatokana na mchanganyiko wa unga huo na ule wa ulezi.

Alisema unga huo unaweza kuwa ufumbuzi kwa wenye uzito uliopitiliza, tatizo linalowakabili Watanzania wengi. Alisema mazao hayo yamebainika kuwa na kiwango kidogo cha sukari na wanga.

"Kwa wagonjwa wa sukari unapokula mtama kuna kemikali inayoitwa 'tanning' ambayo inazuia umeng'enyaji wa virutubisho vingine na kusababisha ule ugali wa mtama kukaa kwa muda mrefu tumboni na husikii njaa.

"Husikii njaa kwa kuwa umeng'enywaji wake unachukua muda mrefu na utaacha kula vyakula vingine vitakavyokusababisha kupata uzito," alisema Dk. Chuwa.

Alisisitiza kuwa mtama ni zao ambalo lina kiwango kidogo cha sukari kulinganisha na mchele na ngano, hivyo ili kupunguza uzito, mtu anatakiwa kula sukari isiyozidi gramu 250 kwa siku kuanzia mlo wa asubuhi mpaka jioni.

Mtaalam huyo alisema mtu anapotumia vyakula vilivyotumia mtama au ulezi kwa siku ataepuka kuongeza kiwango cha kuwa na uzito uliopitiliza.

"Ili kupunguza uzito, inatakiwa mtu ale sukari isiyozidi gramu 250 kwa siku. Hii inamaanisha kuanzia chakula cha asubuhi ukila mkate vipande vitatu ni sawa na gramu hizo 250 inatosha.

"Ukila chapati tatu asubuhi ,mchana ukila ugali wa sembe na jioni wali, kiwango cha sukari kitakuwa kimezidi kwa siku na kukaribisha ugonjwa wa sukari na uzito uliopitiliza," alisema Dk. Chuwa.

Alisema endapo mtu ataendekeza kuwa na utaratibu wa kula, atakuwa anaongeza kiwango cha sukari na kufikia gramu 800 mpaka 1,000 kwa siku.

Dk. Chuwa alisema namna mtu anavyoendelea kula sukari ndivyo anavyokaribisha tatizo la uzito na ugonjwa wa sukari kutokana na kuzidi katika damu na kongosho linashindwa kuondoa sukari ya ziada.

"Ili jambo hili la uzito uliopitiliza lisiweze kutokea, tunatakiwa sasa kurudi kwenye vyakula vya mazao ya nafaka ambayo ni mtama na ulezi, yanayosaidia kuepuka tatizo hili," alisema.

Kuhusu mazao ya mizizi alisema wanahamasisha watu wale viazi mviringo na ndizi hasa wakati wa jioni kwa kuwa vyakula hivyo vina kiwango kidogo cha wanga.

"Endapo utakula vyakula vyenye wanga mwingi na kwenda kulala, ule umeng'enyaji wa sukari unaingia kwa kiwango kingi kwenye damu na hivyo kupata matatizo hayo," alielimisha mtaalam huyo.

Mtafiti huyo alitaja vyakula vinavyoweza kutengenezwa kwa kutumia mtama ili kuepuka uzito kupitiliza kuwa ni kwa kuchanganya mahindi na ngano, jamii ya mikunde yenye protini nyingi ili kuongezea virutubisho na mtu kupata afya bora kwa kutengeneza vyakula kama Togwa, mbege, uji , biskuti, maandazi na mikate.

Mgunduzi wa Mbegu za Mtama kutoka TARI Tumbi mkoani Tabora, Dk. Emmanuel Mrema, alisema zao hilo ni mkombozi kwa mtanzania na wao kama watafiti wanahakikisha wakulima wanapata mbegu bora za teknolojia ya kisasa.

Dk. Mrema ambaye pia ni, Mkurugenzi wa Kituo hicho cha TARI Tumbi, alisema zao hilo linasaidia kutatua changamoto ya mabadiliko ya tabianchi kwenye maeneo mengi yenye mbegu za mahindi ambazo hazifanyi vizuri na kuwa mkombozi wa chakula.

Alisema mtama pia limekuwa mkombozi kwa watu wanaopatwa na tatizo la kiafya kutokana na kuwa na viini lishe vingi vyenye uwezo wa kutatua changamoto za uzito uliopitiliza na magonjwa ya kisukari.

Kuhusu soko la mtama, Dk. Mrema alisema kwa sasa ni kubwa ndani na nje ya nchi na kutolea mfano kwa Tanzania vipo viwanda vya ndani vya bia ambavyo vinahitaji zao hilo na majani yake hutumika kwa ajili ya mifugo.

Kwa upande wa soko la nje alisema nchi za Sudan na Uganda zimekuwa na matumzi makubwa ya mtama unaotoka Tanzania na kuwataka wakulima kuchangamkia fursa zilizopo kwenye zao hilo.

Mratibu wa Kitaifa Programu ya Utafiti Mazao ya Mikunde kutoka TARI Ilonga wilayani Kilosa, Meshack Makenge, alisema ulaji wa mazao ya mikundekunde unasaidia kupunguza tatizo la uzito kwa kuwa una protini nyingi na wanga kidogo kitu ambacho kinasaidia kuepuka na magonjwa yanayotokana na uzito.

Alivitaja vyakula hivyo ni pamoja na dengu, kunde,choroko, soya, maharage ambayo ni mbadala wa kula nyama na vyakula vyenye wanga mwingi kama ugali na wali.



Wauzaji wa chipsi wakifanya biashara kwenye mazingira hatarishi kiafya kutokana na maji machafu yanayotuama na kutoa harufu mbaya katika eneo la Biafla Kinondoni, Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Vilio, simanzi vyatanda wazazi wakipita kuaga mwili bosi ABSA

**Halfani Chusi**

VILIO na simanzi jana vilitanda wakati wazazi wa aliyekuwa Mkurugenzi wa benki ya ABSA, Nechi Msuya (49), wakipita kuaga mwili wake.

Msuya ni mmoja wa wanafamilia wanne waliofariki dunia katika ajali ya gari iliyotokea Chalinze mkoani Pwani. Wazazi hao walipita mbele ya jeneza la mtoto wao kutoa heshima za mwisho katika ibada iliyofanyika kwenye Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT), Usharika wa Kijitonyama, Dar es Salaam, ambayo ilihudhuriwa na mamia ya watu.

Ibada hiyo iliyoongozwa na Mchungaji Kiongozi wa Kanisa hilo, Dk. Eliona Kimaro, katika mahubiri yake, alisema msiba huo ni mzito na kuomba kila Mtanzania kuiombea familia hiyo.

Mchungaji Kimaro alisema kifo ni mpango wa Mungu, hivyo wana familia, ndugu, jamaa na marafiki wanapaswa kulipokea tukio hilo kwa mikono miwili bila kusahau kuwaombea wazazi waliopoteza watoto wao wote wanne.

"Mungu ndiye mwenye kurarua na kuponya majeraha. Mungu aliyeruhusu maumivu kwenye moyo wako ndiye atakayeruhusu shangwe, mambo yaliyofichwa ni ya kwake na yaliyo wazi ni ya kwetu," alisema Dk. Kimaro.

Mchungaji Kimaro pia aliwakumbusha wanaotumia vyombo vya moto kumtanguliza Mungu pamoja na kuzingatia sheria za usalama barabarani ikiwamo kufunga mkanda.

Akisoma wasifu wa Msuya, binamu wa marehemu, Kenneth Lyimo, alisema kijana huyo alikuwa msomi na amefanya kazi katika taasisi mbalimbali za kibenki na ameacha watoto wawili.

Alisema Msuya alikuwa muumini wa dini ya Kikristo na enzi za uhai wake, alikuwa anapenda kushiriki shughuli za kijamii na michezo akikumbushia kuwa alikuwa mchezaji wa mpira wa kikapu.

Lyimo alisema baada ya maziko yanayotarajiwa kufanyika leo, wazazi watarejea Dar es Salaam kwa ajili ya kuaga miili ya ndugu zake wengine, shughuli itakayofanyika Jumanne katika viwanja vya Gofu, Kawe na kwenda kuzikwa katika makaburi ya Kondo Ununio.

Ndugu hao wanne walifariki dunia baada ya gari walilokuwa wakisafiria kugongana uso kwa uso na Scania katika Kijiji cha Mapatano, Mbwewe, Bagamoyo mkoani Pwani.

Ajali hiyo ilitokea Alhamisi saa 8:30 usiku kwa kuhusisha gari lenye namba za usajili T104 CBU Toyota Prado lililokuwa likitokea Dar es Salaam kwenda Same, likiendeshwa na Msuya.

Gari hilo liligongana na lori lenye namba za usajili T881 DWU likiwa na tela lenye namba za usajili 888 DWU likiendeshwa na Philipo Mtisi (43) likitokea Arusha kwenda Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Pwani, Kamishna Msaidizi (ACP) Pius Lutumo alisema chanzo cha ajali hiyo ni dereva wa Toyota Prado kuhama kutoka upande wa kushoto kwenda kulia kisha kugongana na lori hilo uso kwa uso.


**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 84 OF 2023**

**In the Matter of the Estate of the Late:**
**FREDY PAULO LUHIZO**

**By 1. NOVATUS FREDY LUHIZO**
**2. ......................................**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above – named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 31 day of 08/2023

Dated at MOROGORO this 02 day of 08..2023

# Wahariri wafundwa kuimarisha kuhusu usalama, umoja kitaifa

**Na Mwandishi Wetu**

WAHARIRI wa vyombo vya habari waliopatiwa mafunzo katika Chuo cha Taifa cha Ulinzi (NDC) wametakiwa kubadilika, kufikiri kimkakati na kufanya kazi kwa weledi ili kuimarisha usalama na kukuza umoja wa kitaifa.

Kwa kuzingatia hayo, imeelezwa kuwa hawataandika habari zenye uchochezi na uvunjifu wa amani.

Waziri Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Zanzibar, Tabia Maulid Mwita, alisema hayo juzi katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Fatma Hamad Rajab, wakati akifunga kozi fupi ya 15 ya wahariri 59 kutoka vyombo mbalimbali vya habari vya serikali na taasisi binafsi iliyoandaliwa na NDC.

Kozi hiyo ambayo iliongozwa na kaulimbiu isemayo: "Nafasi ya Vyombo Vya Habari Katika Kuimarisha Usalama Na Kukuza Umoja wa Kitaifa", ilitolewa kwa siku tano kuanzia Julai 31, mwaka huu. Miongoni mwa walioshiriki na kutunukiwa vyeti ni Romana Mallya na Beatrice Shayo kutoka Kampuni ya The Guardian na Steven Chuwa wa ITV.

Katika hotuba yake, Mwita aliwataka wahariri kupitia mafunzo waliyoyapata yawasaidie kufanya tathmini ya kina kila wanapohariri na kuchambua habari zenye tija na maslahi mapana ya Tanzania.

"Mwende mkaoneshe tofauti kati yenu na wanahabari ambao hawana kozi hii ili kuifanya nchi ya Tanzania kustawi zaidi," alisisitiza Waziri Mwita.

Aidha, alisema amefurahishwa na chuo hicho kuandaa mafunzo hayo kwa wahariri kwa ajili ya maslahi mapana ya taifa na kulinda umoja wa kitaifa. Alisema mafunzo yamejikita zaidi katika kufanya umahiri mzuri wa habari ili kuimarisha usalama, kukuza umoja wa kitaifa na kuepuka habari zenye uchonganishi au za uvunjaji wa amani.

"Mafunzo haya pia, yamewakumbusha mambo ambayo wahariri wa habari wanatakiwa kuyafanya katika kuimarisha usalama wa taifa letu. Tunategemea kila mshiriki asipoyazingatia atasababisha uvunjifu wa amani kwa jamii yake inayomzunguka na kuhatarisha usalama wa taifa kwa ujumla,"alisema Mwita.

Kiongozi huyo alisema ni wajibu wa kila mhariri kujua uhariri mzuri wa habari ili kuleta maendeleo chanya kwa kizazi kijacho na kilichopo.

Pia alisema mafunzo hayo yatawawezesha kututua changamoto za uhariri zilizokuwa zikiwakabili na zile zinazojitokeza ambazo zinahatarisha usalama wa taifa.

Alisema mhariri mzuri ni yule anayehariri habari zenye tija, uzalendo na zenye maslahi mapana kwa taifa, hivyo kila mmoja anatakiwa kuonyesha utofauti katika utendaji wake wa kazi.

Mwita alisema serikali inatarajia mabadiliko makubwa kutoka kwa wahariri hao kutokana na mafunzo waliyopatiwa katika kuhakikisha nchi inaendelea kuwa na amani, utulivu na upendo.

Aliwataka wakafanye kazi ya kuimarisha usalama na kukuza umoja wa kitaifa kupitia uhariri wao wa habari kwani kufanya hivyo watakuwa wamelitendea haki taifa.

"Tumeona nchi nyingine zinateseka kwa sababu tu ya ulevi wa madaraka na kuingiza nchi katika machafuko. Nchi inavyoingia katika machafuko hata wewe kupata mkate inakuwa shida, hivyo mkawe wahariri bora," alisisitiza.

Katibu Mkuu Fatma alisema amefurahishwa na mafunzo hayo kwa kuwa yamezingatia jinsia na jambo la msingi wanalotakiwa kuzingatia wahitimu hao ni matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili wasikubali kikachezewa.

Alisema wachafunzi wa Lugha ya Kiswahili ni baadhi ya waandishi wa habari, hivyo wanatakiwa kujirekebisha na kuwa wazalendo na lugha yao.Alisema serikali inatambua changamoto zinazowakabili waandishi wa habari na tayari wameanza kuzifanyia kazi kwa kuwa kuna haja ya kuwatazama kwa jicho la huruma kutokana na kazi yao ngumu wanayoifanya katika mazingira magumu na hatarishi.

Mkuu wa chuo cha NDC, Meja Jenerali Ibrahim Mhona, alisema majadiliano yaliyofanyika wakati wote wa kozi hiyo yalikuwa mazuri na jambo la msingi ni kuwajengea uelewa katika kazi zao ili wazingatie maadili na kulinda usalama wa taifa.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji (wa pili kushoto), akipata ufafanuzi wa jambo alipofanya ziara ya kikazi alipotembelea kiwanda cha Maweni Limestone kinachozalisha saruji ya Huaxin, jijini Tanga juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Waagizaji wataja vikwazo vya biashara ya mafuta

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Waagizaji na Wasambazaji wa Mafuta Tanzania (TAOMAC) kimesema uhaba wa Dola ya Marekani katika soko la fedha, umesababisha kupunguza kiasi cha mafuta kinayoagiza kuepuka hasara na kushindwa kulipia tozo mbalimbali.

Hatua hiyo, imesema inaweza pia kusababisha gharama za uendeshaji wa biashara na kuathiri bei ya mafuta kwa mteja.

Kauli hiyo ilitolewa juzi wakati viongozi na wanachama wa TAOMAC walipokutana na Waziri wa Nishati, January Makamba, katika ofisi ndogo za wizara jijini Dar es Salaam.

Katika kikao hicho, TAOMAC ilitoa taarifa ya mwenendo wa biashara ya mafuta duniani na nchini pamoja na kuwasilisha changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ndogo ya mafuta hususani upatikanaji wa dola za Marekani.

Makamu Mwenyekiti wa TAOMAC, Salim Baabde, alisema: "Biashara yetu inafanyika kwa kutumia Dola za Marekani na inapotokea dola inakuwa adimu sokoni, inaathiri moja kwa moja bei ya uagizaji ambayo inaathiri bei ya mafuta kwa mtumiaji wa mwisho".

Alisema, hali inaweza kuwa mbaya iwapo changamoto ya upatikanaji wa dola haitatatuliwa kwa haraka. "Tunaiomba Serikali kuongeza nguvu katika kuhakikisha dola zinapatikana kwa kushirikisha benki za biashara ili kuepuka changamoto hii kukuwa zaidi na kuleta athari kubwa" aliongeza.

Mkurugenzi Mtendaji wa TAOMAC, Raphael Mgaya, alimhakikishia Waziri Makamba kuwa kuwa pamoja na changamoto hiyo, wanachama wataendelea kuagiza mafuta ingawa kwa gharama kubwa ili kuhakikisha nchi inaendelea kupata nishati hiyo muhimu katika hali ya uhakika na endelevu.

"Tutaendelea kuhakikisha tunalinda dhamana tuliyopewa na serikali ya kuhakikisha nchi inakuwa na mafuta wakati wote hata kama ni kwa gharama kubwa" alifafanua.

Viongozi hao walimshukuru Waziri na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kwa ushirikiano ambao wamekuwa wanautoa kwa tasnia hasa katika vipindi vigumu na kuahidi kuendelea kutoa ushirikiano kwa serikali pamoja na kuelimisha umma kuhusu biashara ya mafuta ili kukabiliana na upotoshaji hasa mitandaoni kuhusu biashara hiyo.

Waziri Makamba kwa upande wake aliwashukuru kwa ushirikiano waliutoa kuhakikisha nchi inapata mafuta muda wote huku akiwahakikishia kuwa mlango uko wazi wakati wote kwa ajili ya mashauriano.

"Sisi hapa wizarani falsafa yetu ni ile ya 'open door'. Yeyote anakaribishwa kwa ajili ya mashauriano na majadiliano," alisisitiza.

Aidha, Makamba alisisitiza kuwa serikali inazifahamu changamoto ambazo sekta inakabiliana nazo kwa sasa na kuwa hatua madhubuti zimeendelea kuchukuliwa. Pia, alisisitiza umuhimu wa wadau ikiwamo TAOMAC kuendelea kushikamana na kushirikiana ili kuhakikisha upatikanaji wa mafuta kwa uhakika kwa ajili ya ustawi wa nchi na watu wake.

Kikao hicho kilihudhuriwa na Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, Kamishna wa Petroli na Mafuta, Michael Mjinja, Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dk. James Andilile na wataalamu kutoka Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA).

# NEC yatangaza uchaguzi mdogo ubunge Mbarali, udiwani kata 6

**Na Mwandishi Wetu**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imetangaza ratiba ya uchaguzi mdogo wa ubunge katika Jimbo la Mbarali mkoani Mbeya na udiwani katika kata sita.

MKURUGENZI wa Uchaguzi wa NEC, Dk. Ramadhani Kailima, amesema uchaguzi mdogo wa ubunge Jimbo la Mbarali, na kata sita za Tanzania Bara utafanyika Septemba 19, mwaka huu.

Kailima alisema jana jijini Dodoma kuwa wagombea watachukua fomu kuanzia Agosti 13 hadi 19, mwaka huu, siku ya uteuzi itakuwa Agosti 19 na kampeni za uchaguzi zitaanza siku itakayofuata hadi Septemba 18.

Alizitaja kata zitakazofanya uchaguzi mdogo kuwa ni; Nala (Halmashauri ya Jiji la Dodoma) Mwaniko, Misungwi mkoani Mwanza na Old Moshi Magharibi, Halmashauri ya Wilaya ya Moshi.

Zingine ni Marangu Kitowo katika Halmashauri ya Wilaya ya Rombo, Kilimanjaro, Mtyangimbole iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Madaba na Mfaranyaki Halmashauri ya Manispaa ya Songea, mkoani Ruvuma.

"Tume inatumia nafasi hii kuvikumbusha vyama vya siasa, wagombea na wadau wote wa uchaguzi kuzingatia katiba, sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi, taratibu, miongozo na maelekezo ya tume katika kipindi cha uchaguzi huu mdogo," alisema.

Kailima alisema tume imetoa taarifa hiyo baada ya kupokea taarifa kutoka kwa Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson akiiarifu kuhusu uwapo wa nafasi wazi ya ubunge katika Jimbo la Mbarali.

Alisema nafasi hiyo wazi inatokana na kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo, Francis Mtega na kwamba Spika ametoa taarifa hiyo kwa mujibu wa kifungu cha 37(3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343.

"Tume imepokea taarifa kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa, akiarifu juu ya uwapo wa nafasi wazi za madiwani katika kata sita za Tanzania Bara. Waziri ametoa taarifa hiyo kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292.

"Tume kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 37(1)(b) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 13(3) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, inatoa taarifa kwa umma kuhusu uwapo wa uchaguzi mdogo wa ubunge wa Jimbo la Mbarali na wa madiwani katika kata sita za Tanzania Bara," alisema.



Mkurugenzi wa Kampuni ya Uchimbaji wa Madini ya Rubi ya Sendeu Agrovet Investment Ltd, Gabriel Sendeu Laizer (kushoto), akikabidhi kadi ya gari aina ya Noah kwa Mwenyekiti mstaafu wa kijiji cha Elesin'geta, Kata ya Mundarara wilayani Longido, mkoani Arusha, Akwelino Nikeni kama zawadi kwa ajili ya utendaji kazi wake mzuri wakati wa uongozi wake, katika hafla iliyofanyika kijijini hapo mwishoni mwa wiki. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

## DC ataja siri ndani ya mafuta ya tango

**Na Steven William,** NACHINGWEA

MKUU wa Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, Mohamed Moyo, ametoa wito kwa wanaume kutumia mafuta yanayozalishwa kutokana na mbegu za zao la tango kwa kuwa yanasaidia tatizo la nguvu za kiume.

Akizungumza juzi katika banda la maonyesho la Halmashauri ya Wilaya ya Liwale katika sherehe za Nanenane, alisema mafuta ya zao hilo pia yanasaidia magonjwa ya shinikizo la damu, kisukari na matatizo mengine ikiwamo nguvu za kiume.

Alisema kuwa tango lina mbegu ambazo zinapokaushwa na kukamuliwa, mafuta yake yanasaidia magonjwa mbalimbali.

Moyo alisema tafiti mbalimbali zilizofanywa na wataalam zimeonyesha kuwa mafuta ya tango ndiyo mazuri kwa matumizi ya binadamu kwa sasa.

Alisema kuwa mafuta hayo yanaweza kutumiwa na kila mtu kwa kuwa hayana masharti kama ilivyokuwa kwa mengine na kuwataka wananchi kuyachangamkia.

Baadhi ya wananchi mkoani humo, Charles Mhilu na Fredy Mgunda kwa nyakati tofauti walisema kuwa walikuwa hawafahamu kama mafuta ya tango yanaongeza nguvu za kiume.

# Wenye ualbino wataka mkazo sheria ya ajira wenye ulemavu

**Na Vitus Audax,** MWANZA

BAADHI ya vijana wenye ualbino, wameiomba serikali kutilia mkazo katika utekelezaji wa sheria ya waajiri kuwa na asilimia tatu ya watu wenye ulemavu katika taasisi zao.

Hali hiyo, wamesema itawasaidia vijana wenye ujuzi na sifa za kuajiriwa kuendelea kupata fursa ili kujikwamua kiuchumi.

Vijana hao wanaodhaminiwa masomo katika ngazi zote za elimu na shirika lisilo la kiserikali la Under The Same Sun (UTSS) walitoa ombi hilo jana kwa nyakati tofauti wakiwa katika kambi ya pamoja iitwayo Kempu ya Majira ya Joto iliyowakutanisha zaidi ya watu wenye ualbino 240.

Licha ya kutoa pongezi zao kwa serikali kuendelea kuona haja ya kutoa fursa za ajira kwa vijana hao katika ngazi mbalimbali, walisema changamoto bado ipo katika sekta binafsi ambayo imekuwa ikishindwa kutekeleza takwa hilo la kisheria kwa visingizio mbalimbali. "Mara nyingi waajiri wamekuwa wakitutenga kuanzia kwenye usaili ambako hata namna ya usaili unavyofanyika unaona kuwa hii ajira hutakiwi kabisa, hivyo serikali iweke mkazo vijana wenye vigezo wapewe ajira," alisema Christina Sylas.

Faudhia Kitenge, kijana mwenye ualbino na mwanafunzi wa shahada ya uzamili na mkufunzi msaidizi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, alisema licha ya baadhi ya watu wenye ulemavu kuwa na uwezo kiutendaji, wamekuwa wakishindwa kufikia ndoto zao kutokana na kutokuaminiwa na waajiri.

"Waajiri wengine wanasema endapo tukimwajiri mtu huyo atatugharimu kwenye mambo ya kumuhudumia. Kwa mfano sisi wenye ualibino wanasema tutahitaji huduma za ziada lakini kiuhalisia si kweli kwani tunajua namna ya kujihudumia," alisema. Yassin Kasiga, ambaye licha ya kuwa mwenye ualbino pia ni ofisa habari katika Halmashauri ya Wilaya Itigi, alisema licha ya serikali kuweka sheria inayowapa unafuu wenye ulemavu, bado kuna haja ya serikali kufanya ufuatiliaji kuhakikisha sheria hiyo inafuatwa.

"Hatuhitaji kuajiriwa kwa kuonewa huruma lakini lazima kila anayekidhi vigezo na ameomba kazi apewe kipaumbele na serikali itazame wale wasiotekeleza sheria hiyo," alisema Kasiga. Mratibu wa Kempu ya Majira ya Joto kutoka UTSS, Grace Wabanhu, alisema wamekuwa wakiwafadhili kimasomo watoto wote wenye ualbino pamoja na wenzao walioathirika katika kipindi cha mauaji ya albino kuanzia ngazi ya msingi mpaka watakapotosheka na elimu.

Licha ya kufanya hivyo, alisema wamekuwa wakiwapa mafunzo wanafunzi hao kuendana na ujuzi wao ili kukidhi vigezo vya kuajiriwa katika sekta binafsi na serikalini.

"Tunahakikisha pia tunakutana na waajiri lengo ni kuwapa uelewa juu ya uwezo walio nao vijana hawa ili waache kuwapima kulingana na hali zao ikiwa ni pamoja na kuwaombea ajira za muda ambazo zitawasaidia kuaminiwa na waajiri," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Jitihada zaidi zinahitajika kuzalisha wahandisi wa kike

**KWA** miaka mingi wanawake walikuwa wakiwekwa nyuma katika nyanja mbalimbali kutokana na mfumo dume uliokuwa umetawala katika jamii. Hatua hiyo ilisababisha kukosa fursa mbalimbali zikiwamo za uongozi pamoja na elimu.

Yote hiyo ilitokana na fikra zilizojengeka kuwa kazi kubwa ya mwanamke ni kuolewa na kulea mtoto.

Pia, baada ya kuolewa, katika baadhi ya makabila, walikuwa wakipewa zana za kilimo na mapipa kwa ajili ya kupikia pombe jambo ambalo lilikuwa likimaanisha kwamba mwanamke baada ya kuolewa, anatakiwa kuzalisha mali na baada ya kuvuna mazao, apike pombe na kuuza ili kupata fedha kwa ajili ya kulisha familia.

Mfumo huo dume haukuishia hapo bali hata baada ya kuvuna mazao aliyoyavujia jasho shambani pamoja na pombe alizokuwa akipika ili kupata fedha kwa ajili ya kutunza familia, mwanamke alikuwa hana mamlaka ya kutunza fedha hizo.

Wakati mwingine mume alikuwa anachukua mazao hayo na kuuza kisha fedha kuzitumia kwa jinsi alivyoweza bila hata kuulizwa.

Miaka ya hivi karibuni, liliibuka vuguvugu la ukombozi wa wanawake lililolenga kuwapo kwa usawa wa jinsia katika mgawanyo wa rasilimali, uongozi na uwajibikaji katika maeneo mbalimbali. Matokeo ya vuguvugu hilo yanashuhudiwa hivi sasa kutokana na wanawake kupewa haki sawa zikiwamo za uongozi. Hivi sasa katika maeneo mbalimbali wanawake wameshika nafasi za uongozi zikiwamo za juu kwenye uongozi wa taasisi na nchi kwa ujumla.

Pamoja na matokeo hayo chanya, bado kuna uhaba wa wanawake wataalamu katika nafasi mbalimbali hasa zile za taaluma za kisayansi kama vile afya, uhandisi, sayansi na teknolojia. Suala hilo halijaangaliwa kwa jicho la ndani licha ya kuonekana kwamba katika uongozi, Tanzania kwa mfano, kuna dalili njema za kufikia uwiano wa 50 kwa 50.

Suala la uhaba wa wanawake katika utaalamu hasa kwenye sayansi liliibuliwa kwenye mkutano wa mwaka wa wanawake wahandisi uliofanyika Zanzibar. Mfano ulitolewa katika Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) kwamba wahandisi wanawake walioko kwenye taasisi, wameonyesha uwezo mkubwa katika utendaji kazi licha ya kuwa ni wachache kulinganisha na wanaume.

Mkurugenzi Mkuu wa TARURA, Mhandisi Victor Seff, alisema wanawake wahandisi ndani ya taasisi hiyo, waliopewa nafasi za uongozi wameonyesha umahiri hata kuwashinda wanaume lakini kikwazo kikubwa ni idadi ndogo.

Mkurugenzi mkuu huyo aliweka bayana kwamba katika taasisi hiyo ambayo ina ofisi katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara, wahandisi wanawake ni 400 kati ya 1,700 sawa na asilimia 13. Kiwango hicho kinaonyesha kwamba bado kuna kazi kubwa ya kufanya katika kufikia mafanikio na usawa wa kijinsia kitaaluma hususan katika fani za sayansi.

Ni dhahiri kwamba wako wanawake mahiri katika fani za sayansi zikiwamo udaktari, famasia, uhandisi, kompyuta na mawasiliano lakini bado idadi yao ni ndogo kulinganisha na wanaume.

Kwa mantiki hiyo, jitihada za makusudi zinatakiwa kufanyika ili kuwa na wahitimu na wataalamu mahiri wa sayansi katika maeneo mbalimbali ili kufikia uwiano sawa wa kijinsia katika nyanja mbalimbali.

Tunatambua kuwa kumekuwa na ufadhili wa masomo ya sayansi ukiwamo ule wa Rais Samia Suluhu Hassan ambao unatoa nafasi kwa wasichana kujiunga na kusomea masomo ya sayansi jambo ambalo ni la kupongezwa.

Hata hivyo, jitihada zaidi zifanyike kwa taasisi mbalimbali kutoa nafasi za ufadhili kwa watoto wa kike kujiunga na masomo ya sayansi ili kuongeza idadi ya wanawake wataalamu katika fani hizo masomo ya sayansi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wanasiasa msivunjiane heshima kujadili uwekezaji bandarini

Na Sabato Kasika

**VYAMA** vya siasa vya CCM, CHADEMA na ACT- Wazalendo, vinaendelea na mikutano ya hadhara katika mikoa mbalimbali, kumwaga sera na kujitafutia wanachama wapya na mashabiki wa kuviunga mkono.

Mikutano ya hadhara ambayo ilikuwa imezuiwa tangu mwaka 2016, ilifunguliwa na Rais Samia Suluhu Hassan mwanzoni mwa mwaka huu na kuvifanya vyama kuanza kuzunguka maeneo mbalimbali nchini.

Hadi sasa vinaendelea kuendesha mikutano hiyo ambayo ni kama imetekwa na hoja ya mkataba wa uwekezaji katika Bandari ya Dar es Salaam, huku kila chama kikiwa na mtazamo wake tofauti.

Wapo viongozi wa vyama hivyo wanaoukubali mkataba huo na wengine wanaukataa, huku kila upande ukiwa na hoja zake zinazoelezwa kwa wananchi kila sehemu ambayo kunafanyika mikutano hiyo.

Kimsingi ni kwamba, katika mikutano hiyo kuna upande unaelezea uzuri wa mkataba huo na mwingine unaelezea ubaya wa mkataba. Yaani kila upande unavutia kwake kwa hoja mbalimbali.

Hata hivyo, uwasilishaji wa hoja za wanasiasa hao kuhusu mkataba huo, umekuwa na ukakasi, ambao ninadhani unaweza kusababisha mkanganyiko kwa hao wanaokwenda katika mikutano yao kuwasikiliza wakimwaga sera.

Ninadhani ni busara kutumia lugha ya staha kufikisha ujumbe, kutoa maoni au kuchambua jambo, kwani watu wanaweza kuelewa vizuri kuliko njia wanayotumia sasa ya hoja ya nguvu badala ya nguvu ya hoja.

Sidhani kama ni sahihi kulazimisha hoja kwa kutumia maneno ya kejeri, kashfa na hata matusi, kwani kufanya hivyo si kufafanua hoja bali inaweza kuwa sawa na kuwachanganya wanaokusikiliza wasielewe mjenga hoja anachotaka.

Kwa mtindo unaoendelea sasa, ninadhani mjadala wa uwekezaji wa bandari, unaweza ukaisha bila wananchi kuelewa ni nani yuko sahihi, kwani sehemu kubwa ya hoja za wanasiasa inaonekana ni 'kushambuliana'.

Hili suala la uwekezaji, lingefaa liwe fundisho la kuwafanya wanasiasa waachane na siasa za aina hizo ambazo wengine huziita siasa za majitaka, badala yake wajinadi kwa hekima, busara na kujenga hoja zenye mashiko.

Ikumbukwe kuwa kwa kawaida mtu anapoishiwa hoja, hugeuka na kuanza kutoa lugha isiyofaa. Hivyo wanasiasa wanaotumia lugha hizo wangetafakari na kisha kuchukua hatua zitakazowafanya wawe na nguvu ya hoja.

Sitaki kuamini kwamba wanasiasa wameishiwa hoja, bali inawezekana wamekengeuka kidogo, hivyo ingependeza kama watarudi kwenye mstari na kufanya siasa za kistarabu badala ya majitaka.

Wananchi nao wana uelewa wa kutosha, wanajua kuchambua hoja mbalimbali, kwa maana hiyo suala la umakini katika uwasilishaji wa hoja ni la muhimu kwani wanaweza kuvutika nao au wakakimbia.

Hivyo, suala la wanasiasa kukosoana halikwepeki lakini kinachotakiwa kuzingatiwa ni namna ya ukosoaji usiwe wa kudhalilisha upande mwingine bali unaojikita kwenye hoja za msingi zinazojadiliwa.

Ni miaka mingi tangu nchi iliporejea katika mfumo wa vyama vingi vya siasa lakini bado wapo baadhi ya wanasiasa ambao badala kutetea maslahi ya taifa kwa hoja nzito wanaegemea kwenye hoja za nguvu.

Wawe wanasisa wa chama tawala au upinzani, ninaamini lengo lao ni moja la kuijenga Tanzania lakini wanapoacha lengo hilo na kugeukia mambo ya 'kushambuliana' majukwaani, ninadhani wanawakatisha tamaa wananchi.

Matumizi ya lugha ya staha katika uwasilishaji wa hoja yanaweza kufikisha ujumbe kwa wananchi na ukaeleweka vizuri, kwani vinginevyo wanaotumia lugha kali wanaweza kutasifriwa kuwa wanalazimisha jambo.

Kutumia maneno makali kama wanavyofanya baadhi ya wanasiasa, ninakuchukulia kama kulazimisha jambo, na ndipo linapokuja neno hoja ya nguvu, badala ya nguvu ya hoja. Wote wana lengo la kujenga Tanzania, ingependeza kama watashindana kwa nguvu ya hoja.

## FIKRA MBADALA

# Umefika wakati wa kutimiza ndoto za Mwalimu Nyerere



Pascal Mayalla

HUU mjadala wa IGA ya DP World na bandari zetu, bado unaendelea japo umetugawa katika makundi mawili ya wanaounga mkono na wanaopinga. Naomba kusisitiza hakuna anayepinga uwekezaji wa bandari yetu ili ifanye kazi kwa ufanisi zaidi. Upinzani ni kwenye ufinyu tu wa uelewa na hoja za kisheria kuhusu mkataba huo ambao wiki iliyopita, niliuita ni barua ya posa.

Hoja za mkataba huu au makubaliano haya na mjadala huu, kiukweli unatusaidia kwa mengi.Sasa kuna watu wanaanza kuhoji serikali ya Tanganyika, wanataka serikali tatu.

Baadhi ya Watanzania wanahoji Muungano na kuitaka serikali ya Tanganyika! Naomba kutangaza maslahi, kwenye hoja za Muungano, mimi ni mfuasi wa falsafa ya Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere ya Umajumui wa Afrika (Pan Africanism) ya kuunganisha bara la Afrika kuwa nchi moja, mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuelekea kwenye shirikisho la Afrika Mashariki la kuwa nchi moja.

Kabla ya Muungano, Tanganyika na Zanzibar zilikuwa nchi mbili, mwaka 1964 zikaungana na kuwa nchi moja ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT), hivyo wengi wetu ni Watanzania. Watanganyika ni wale wazee waliozaliwa kabla ya mwaka 1964, hivyo haiwezekani mtu uzaliwe Tanzania, halafu leo uanze kuitaka Tanganyika.

Muungano wa nchi mwaka 1964 ulifuatiwa na muungano wa vyama vya TANU na ASP vilipoungana mwaka 1977 na kuzaliwa Chama Cha Mapinduzi (CCM). Pia si wengi humu walikuwa wamezaliwa.Waliozaliwa baada ya hapo wameikuta CCM, hawakuikuta TANU na ASP, hivyo hawajui kwa nini TANU na ASP viliungana ili iweje. Sababu ya TANU na ASP kuungana ni kuelekea kwenye serikali moja. Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere alisema huu muungano wa vyama vya TANU na ASP na kuzaliwa chama kipya - CCM, ni mwanzo wa safari ya kuondoka kwenye muungano wa serikali mbili, kuelekea kwenye muungano wa serikali moja. Je, sasa umefika wakati wa kutimizwa kwa ndoto hii ya Mwalimu Nyerere, kwa Tanzania kuwa nchi moja yenye serikali moja na rais mmoja, itakuja kutimia?

Wakati tukijiandaa kusherehekea miaka 60 ya Muungano, Aprili 26, 2024, Watanzania wanahitaji sana kuelimishwa kuhusu Muungano, tena ni Rais wa sasa, Samia Suluhu Hassan, ndiye aliyetoa ruhusa watu waachwe huru kujadili Muungano. Akiwa makamu wa Rais, Samia aliwahi kunukuliwa akisema: "Watu waachwe huru kuujadili Muungano." Sasa nadhani umefika wakati wa kufanya hivyo ili kuwafanya Watanzania wapate elimu na hatimaye kuwa na uelewa mpana kuhusu Muungano.

Elimu inayotakiwa kuhusu Muungano wetu adhimu ni lazima iwakumbushe Watanzania kuwa duniani kuna miungano ya aina mbili kuu. Kwanza muungano unaoitwa 'Union'. Katika aina hii ya muungano,nchi mbili au zaidi zinaungana kuunda nchi moja. Zile nchi zote zinakufa na inazaliwa nchi moja mpya.

Aina ya pili ni muungano wa shirikisho (federation) aina hii ya muungano nchi mbili au zaidi zinaungana na kuunda nchi moja lakini zile nchi zote zinakuwa na serikali ya muungano (Federal Government) na serikali za majimbo, yaani kila nchi inakuwa na utawala wake wa ndani.

Muungano wetu ulitokana na Tanganyika na Zanzibar ni wa aina ya kipekee (unique) kwa sababu ni muungano pekee duniani ambao kwa upande mmoja ni muungano wa nchi mbili kuungana kuunda nchi moja - Tanzania, na kwa upande wa pili ni muungano wa shirikisho wenye serikali mbili.

Muungano wetu kimataifa ni muungano wa 'union'. Tanzania kimataifa ni nchi moja ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT) yenye serikali moja ya JMT chini ya Rais mmoja wa JMT ambaye ni mkuu wa nchi (head of state), mkuu wa serikali (head of the government) na Amiri Jeshi Mkuu.

Lakini kitaifa, Tanzania ni nchi moja ya JMT yenye sehemu mbili, Tanzania Bara na Tanzania Visiwani au Tanzania Zanzibar, yenye katiba mbili. Katiba ya JMT na katiba ya Zanzibar. Nchi yenye serikali mbili, yaani serikali ya JMT na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), yenye marais wawili - Rais wa JMT na Rais wa Zanzibar

Kutokana na kuwapo kwa aina hiyo ya Muungano na seriakli mbili, kuna mkanganyiko wa katiba kati ya ile JMT ya mwaka 1977 na katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, ambao nitaufafanua kwa kina kwenye makala ya wiki ijayo.

**HITIMISHO**

Baada ya Rais Samia kuifungua nchi, kuurejesha uhuru wa kujieleza na hadi kuturuhusu kuujadili muungano, tunapofanya maandalizi ya Katiba mpya, Watanzania waelimishwe kuhusu katiba na muungano. Na kwa maoni yangu, dawa pekee ya uhakika na ya kudumu ambayo ni mwarobaini wa kutibu na kuzimaliza kabisa kero zote za Muungano, sio kwenda kwenye serikali tatu, bali kwenda kwenye serikali moja.

Kwa mujibu wa kitu kinachoitwa kwa lugha ya Kiingereza, 'the political dynamics' ya siasa zetu, kutokana na mjadala wa serikali moja kuwa nyeti sana kwa upande mmoja, huu ndio wakati bora wa kulijadili hili.

Nimalizie na swali je, Tanzania sasa mmefika wakati wa kutimiza ndoto ya Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere ya uzalendo wa kweli wa nchi yako ya JMT wa kwenda kwenye serikali moja?

**Wasalaam,**
**Paskali.**
**+255 754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Viongozi Rais Samia si roboti tumsaidie!



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

KUNA picha imekuwa ikisambaa sana kwenye mitandao ya kijamii, ikionyesha mabaki ya vifaranga wa ndege waliofia kwenye tundu au kiota chao wakisubiri chakula.

Ukichunguza sana walivyokufa vifaranga wale mpaka kubaki mifupa, utagundua kuwa kabla ya mauti kuwakuta, walilia sana kwa njaa wakitarajia mama yao angefika na vipande vya nyama au wadudu ili kuwalisha.

Lakini kwa bahati mbaya inawezekana mama ndege huko mawindoni alikokuwa naye aliwindwa ama na binadamu, wanyama au ndege wengine wakubwa waliomzidi nguvu.

Kwa hali hiyo, vifaranga wale walizidiwa na kupoteza maisha huku wakiwa vinywa wazi, vilivyokuwa vikisubiri mama yao kuvijaza kwa chakula. Walikufa wakakauka na kubaki mifupa.

Hali ile inaonesha jinsi ambavyo maisha yao yalimtegemea mama na hakuna jirani aliyejali kuwasaidia kwa chakula, na pengine kila waliposikia mchakato hata wa upepo, walidhani ni mama karudi na chakula na kuachama.

Hiyo ndiyo sababu iliyochangia kufa wakiwa vinywa wazi. Inaonesha pia jinsi kina mama walivyo muhimu katika maisha ya familia, bila wao hakuna maisha, iko hivyo kwa wanyama na hata binadamu. Mama hupata uchungu sana anaposhuhudia mwanawe ana matatizo.

Picha ile ina mafunzo mengi kwetu sisi binadamu na hususani Watanzania tunaoongozwa na mama. Tunaongozwa na Rais mwenye umbile la kike lakini anayeonyesha upendo na uvumilivu akitaka kuona sisi vifaranga tukipata riziki kwa usawa.

Kwa kulitambua hilo, ndiyo maana katika kila kona ya nchi, utasikia wananchi wenye matatizo wakimwomba Rais Samia Suluhu Hassan aingilie kati kuwasaidia.

Utaona kila waendako viongozi wa chini kuonana na wananchi, mabango yakihanikiza maombi kwa Mama asaidie kutatua matatizo yaliyopo kana kwamba hao viongozi hawawezi.

Kama siku ile angetokea ndege mwingine na kuwaona wale vifaranga wakilia kwa kukata tamaa vile pengine angewasaidia kwa chakula na maafa yale yasingewakuta.

Lakini yawezekana walipita ndege katika mti ule na karibu na tundu lile, lakini wakajali zaidi matumbo yao na kuacha vifaranga waangamie kwa sababu tu hawakuwa wa uzao wao.

Wananchi wanamlilia Rais Samia awatatulie matatizo yao, huku wakiwa na viongozi wao wa maeneo, mawaziri, wakuu wa mikoa, wilaya, tarafa, kata na vijiji, inaashiria nini? Kutowajibika! Endapo viongozi hao wangeona wananchi wakitatizika na kulalamika, bila shaka wangechukua hatua na isingekuwa kazi tena ya Rais Samia kuwazungukia kusikiliza kero zao huku akiwakilishwa.

Tatizo ni kwamba baadhi ya viongozi wanajua kuwa wakishapewa majukumu kwa kuteuliwa au kuchaguliwa, basi moja kwa moja hutumia fursa hiyo kujinufaisha na kujineemesha.

Tunawaona viongozi wanavyopiga kampeni nyakati za uchaguzi wakipiga magoti na kutoa shikamoo hata kwa wadogo zao, huku wakitoa ahadi kemkem za kuwasaidia lakini baada ya ushindi na kuchaguliwa, hupotea.

Husubiri unapokaribia uchaguzi mwingine na kuja kunyenyekea huku wakiwa na magari ya kifahari waliyoyapata kutokana na kura walizopigiwa na kupotelea kusikojulikana na kujali mambo yao binafsi.

Rais anabebeshwa mzigo mzito ambao ungepunguzwa uzito na wawakilishi wake, ambao baadhi yao hujivika umungumtu na kuonekana kuwa na nguvu hata wakati mwingine kumzidi aliyewateua na kutesa wananchi.

Sasa hivi tunashuhudia Rais akirushiwa maneno ya shombo na baadhi ya watu kwa sababu tu ya 'mkataba' wa DP World huku wasaidizi wake ambao wangesaidia kuelewesha wananchi, wakijificha kuchelea kuumbuliwa.

Ndio wale wanaosikilizia upepo, wakiona unavuma vizuri basi hujifanya kuwa karibu na Rais lakini ukivuma vibaya hujificha na kujifanya hamnazo ili tu kufurahisha upande mwingine. Tumsaidie Rais kutekeleza dhima yake kwa jamii anayoiongoza na tumwoneshe imani yake kwetu na yetu kwake, kwa sababu yeye kama yeye hawezi kumaliza matatizo yote yaliyomo nchini.

Tuachane na unafiki wa kusema Mama katoa mabilioni ya fedha kwa hili na lile, huku tukishindwa kuyasimamia katika kusaidia kuleta maendeleo ya watu na kusababisha malalamiko yasiyokwisha leo hata kesho.

Tuhakikishe tunakuwa ndege wenye huruma kiasi kwamba tukibaini vifaranga wanakufa njaa tunduni, basi tuwahi kuwasaidia si mpaka kumsubiri mama afike na vipande vya nyama au wadudu.

Mama anaweza kuwa na majukumu mengine na kushindwa kufikia kila kifaranga kilichoko tunduni na matokeo yake vifaranga wanaathirika vibaya na hatimaye Mama kuonekana mzembe na kumbe sivyo. Alamsiki!

## Usambazaji dawa za MSD Mafia wapunguza rufani wagonjwa Dar

**Na Mwandishi Wetu**

BOHARI ya Dawa (MSD) imesema usambazaji wa dawa na vifaa vya kisasa kisiwani Mafia, umepunguza rufani za wagonjwa kutoka kisiwani humo kwenda kutibiwa Dar es Salaam.

Ofisa Huduma kwa Wateja wa MSD, Diana Kimario, alisema juzi bohari hiyo imepunguza rufani za wagonjwa kutoka kisiwani Mafia kwenda Dar es Salaam kwa kufunga vifaa tiba vya kisasa hususani vya maabara na upasuaji.

"Wilaya hii ina vituo vya afya 25 ambapo vituo 21 vipo Mafia na vituo vinne vipo katika visiwa vidogo, ambapo vifaa vilivyosambazwa na MSD vitafanikisha kupunguza changamoto ya rufani kwa wagonjwa waliokuwa wakisafirishwa kwenda jijini Dar es Salaam kwa ajili ya huduma," alisema.

Pia alisema wamesambaza mashine za X-ray, vitandaa vya kuchangia damu, mashine za kusaidia upumuaji, jenereta kubwa na ndogo na vifaa vingine vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 450," alisema.

Kimario alisema hatua hiyo imefikiwa kutokana na maboresho makubwa yaliyofanywa na serikali kwa hospitali kuwa na majengo ya kisasa yanayokidhi vifaa vilivyofungwa hususani jengo la dharura na wagonjwa mahututi (ICU).

Alisema pamoja na mafanikio hayo, kuna changamoto ya usafirishaji wa dawa na vifaa tiba kutokana na tozo wanazokutana nazo bandarini na kuiomba serikali kuona namna ya taasisi husika ikiwamo wilaya, MSD na bandari kukaa pamoja na kutoa msamaha kwa bidhaa za afya.

"Kuleta gari ya dawa na vifaa tiba Mafia ni gharama unalipia kivuko na kodi kwa bandari na Nyamisati na Mafia na iwapo tutashindwa kulipia inatulazimu kushusha mzigo na kupakia katika meli na wanapofika Mafia kutafuta gari ndogo za serikali au za kukodi kusambaza ambapo usambazaji unachukua muda mwingi," alisema.

Naye Mganga Mkuu wa Wilaya ya Mafia, Dk. Maulid Majala, alisema hospitali hiyo imepokea zaidi ya Sh. milioni 550 kwa ajili ya ujenzi wa majengo mapya mawili na Sh. bilioni 1.39 kwa ajili ya vifaa tiba na kutoa wito kwa watumishi kuhakikisha uwekezaji huo unaendana na thamani ya huduma zinazotolewa.

Alisema ujenzi wa majengo hayo na vifaa vya kisasa ni muhimu kwa kuwa awali walikuwa wakikutana na wagonjwa wa dharura hususani wa ajali inawaladhimu kuwapa rufani kutokana na hospitali hiyo kukosa vitendea kazi.

Dk. Majala alieleza ujio wa bidhaa hizo za afya na upatikanaji wa dawa kutoka asilimia 60 hadi 90 umeboresha utoaji wa huduma kisiwani Mafia.

Naye Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Mafia, ambaye ni daktari bingwa wa wanawake, Dk. Said Maya, alisema kutokana na mazingira ya kisiwa hicho, wanaishukuru MSD kwa kazi kubwa inayoifanya kuhakikisha dawa na vifaa tiba vinafika hadi vituoni bila kujali changamoto za mazingira yalivyopo.

# Waziri ahimiza viwanda ubora bidhaa

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, ametaka viwanda vyote nchini kutengeneza bidhaa zenye ubora kwa gharama nafuu ili kuingia katika Soko la Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA)

Waziri Kijaji aliyasema hayo juzi alipotembelea Kiwanda cha kuzalisha maziwa cha Tanga Fresh kilichoko jijini Tanga kwa lengo la kujionea shughuli za uzalishaji wa maziwa na kusikiliza na kutatua changamoto walizonazo.

Alisema serikali inafanya jitihada mbalimbali kuhakikisha wafanyabiashara na wawekezaji wanakuwa na mazingira bora na wezeshi ili kufanya biashara kwa tija na kukuza uchumi wa Taifa.

Pia alisema, alisema dhamira ya serikali nikuona wafugaji wanabadilika kutoka katika ufugaji wa kienyeji kwenda katika uwekezaji wa kisasa ili kukidhi mahitaji ya soko.

Waziri alikipongeza kiwanda hicho kwa ajira walizotoa hapa nchini na kuongeza kuwa wafanye bidii kuhakikisha ajira zisizo za moja kwa moja zinaongezeka.

Wakati huo huo, Waziri Kijaji alisema serikali itahakikisha sekta binafsi inaendelea kukua na hakuna kiwanda chochote kitakachofungwa ili kuendelea kuongeza ajira na kukuza uchumi wa taifa

Aliyasema hayo wakati alipotembelea Kiwanda cha A to Z kilichoko jijini Arusha kwa lengo la kujionea shughuli za uzalishaji kiwandani hapo, kusikiliza na kutatua changamoto walizonazo.

Aidha, aliwataka wafanyabiashara kushirikiana na Serikali kwa kueleza changamoto wanazopata na watoe mapendekezo ya suluhisho za changamoto hizo kwa kuwa Serikali ipo tayari kuzishughulikia.

Waziri Kijaji pia alisema serikali itahakikisha inakisaidia kiwanda cha kutengeneza vipuri Kilimanjaro (KMTC) kufikia malengo katika masoko kwa kuwa dhamira ya Serikali ya ni kuona uzalishaji wa ndani unafanyika kupitia chuma kinachozalishwa nchini.

Aliyasema alipotembelea kiwanda hicho na aliwapongeza wafanyakazi wa kiwanda hicho na kuwataka wawe waaminifu kwa kwani serikali inafanya jitihada mbalimbali za kuweka mazingira bora ya biashara ili kuvutia wawekezaji katika viwanda vitakavyotumia vipuri vinavyotengenezwa na kiwanda hicho.

Kadhalika, Waziri Kijaji alikutana na wafanyabiashara wa jiji la Tanga na kushauri uongozi wa mkoa huo kushirikiana na taasisi husika kutatua changamoto wanazopata wafanyabiashara wa jiji la Tanga.

Alisema dhamira ya Serikali nikurudisha jiji la Tanga kuwa la viwanda nchini kama hapo awali ili liweze kutoa ajira kwa vijana kukuza biashara na uchumi wa taifa .

Dk. Kijaji pia aliishauri Mamlaka ya mapato Tanzania (TRA) isiwabebeshe mzigo wafanyabiashara kwa kulimbikiza kodi bali ishirikiane na wafanyabiashara hao na kuwapa elimu kuhusu umuhimu wa ulipaji kodi kwa hiari.



Mbunge wa Jimbo la Nachingwea, mkoani Lindi, Dk. Amandus Chinguile (kulia), akikabidhi kadi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa mmoja kati ya wanachama wapya 36 waliohamia chama hicho kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wakati wa mkutano wa hadhara katika Kijiji cha Naipanga, jimboni humo juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Watanzania washauriwa kutumia umeme jua

**Na Dennis Fussi**

WATANZANIA wameshauriwa kutumia nishati ya umeme jua (solar energy) nyumbani, ofisini na viwandani ili kuwa na uhakika wa nishati hiyo ambayo gharama yake ni ndogo na hudumu kwa muda mrefu.

Akizungumza mara baada ya kuibuka kuwa washindi wa pili katika utoaji wa huduma bora ya nishati ya jua nchini (Solar Company of the Year Award), Mkurugenzi Mtendaji wa Compact Energies, kampuni ya usambazaji na ufungaji wa vifaa vya umeme jua, Ephraim Kimati alisema wamekuwa mstari wa mbele katika kuleta mageuzi ya nishati hiyo katika maeneo mbalimbali.

Tuzo hiyo ilitolewa wakati wa utoaji wa tuzo za Kampuni Bora ya Mwaka ya Afrika (Africa Company of the year (ACOYA) katika ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam juzi. Kimati alisema gharama za mwanzo za kupata umeme jua zinaweza kuwa ni kubwa, lakini baada ya hapo matumizi huwa ni ya zaidi miaka 20 au 30 bila gharama nyingine zozote.

"Niwahimize Watanzania kutumia mfumo wa umeme jua kwa sababu si gharama lakini unasaidia kuokoa gharama," alisema.

Alisema mwelekeo wa dunia kwa sasa ni kutumia mfumo wa umeme jua na gesi na nchi nyingi Ulaya na Afrika zikiwemo zile za G7 zinasisitiza matumizi ya nishati hiyo ili kuleta maendeleo ya haraka hasa katika maeneo ya vijijini.

Kimati alitoa wito kwa Watanzania kununua huduma zinazotolewa na makampuni ya nyumbani ili kukuza soko kwa maendeleo ya nchi na kukuza nguvu ya uchumi kwa nchi za Afrika ili kushindana katika soko la dunia.

Alisema wakiwa kampuni ya wazawa, wamefanya kazi kwa ufanisi katika miradi mbalimbali ukiwemo wa bomba la mafuta ghafi la Afrika ya Mashariki (EACOP) ambapo wao ndio walifunga mfumo mzima wa nishati ya jua katika nyumba walizopewa watu fidia na mradi huo mkubwa.

"Tumepata mrejesho mkubwa sana kutoka kwa watu tuliowahudumia na hata wakati tulipowakabidhi mfumo wa sola walifurahia sana. Tuna vifaa vya kisasa na wafanyakazi wenye weredi na kujitoa ili kuwapa Watanzania huduma bora, zenye unafuu na uhakika. "Kiukweli tunaona mchango wetu mkubwa katika jamii ya Watanzania kwa kuwapa huduma ya nishati watu ambao walikuwa hawana uhakika wa umeme na hata wale ambao wamefunga kwa ajili ya kuhakikisha hawapati changamoto hata umeme ukikatia," aliongeza.

Mkurugenzi wa tuzo hizo zilizoandaliwa na zilizoandaliwa na Estern Star Consulting Group, Deogratius John, alisema lengo la kuanzisha tuzo hizo ni kutambua ushindani wa kibiashara wa Afrika kwa makampuni ya Afrika ili yapate utambulisho katika soko la dunia.

Alisema ushindi wa tuzo hizi zinayafanya makampuni kuaminika katika soka na kuonyesha uwezo wao katika kutoa huduma.

John aliongeza kuwa ana imani makampuni ya Tanzania na Afrika kwa ujumla yana uwezo wa kushindana na makampuni ya nje yaliyowekeza katika teknoloji, licha ya biashara inayofanyika ndani ya Afrika ni ndogo, ukilinganisha na biashara ambayo Marekani au China inafanya na nchi za Afrika.

Katika tuzo hizo zilizohusisha makampuni na mashirika kwenye zaidi ya vipengele 80 ambapo ASA Microfinance ndio walikuwa vinara wa tuzo hizo.

# MAISHA

AGOSTI 6, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili




Ukurasa 13

**Jaribu upende**



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Tumia gharama kidogo katika kubadili mwonekano wa nyumba



Ukurasa 12

**HARUSI**




# Kicheko kinanoga

Ukurasa 14

## WATOTO


### MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA




| | | | |
|---|---|---|---|
| 3 | 1 | 4 | 2 |
| 4 | 2 | 3 | 1 |
| 1 | 3 | 2 | 4 |
| 2 | 4 | 1 | 3 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| M | ■ | F | U | N | D | A |
| A | ■ | ■ | ■ | U | ■ | M |
| K | ■ | T | I | N | ■ | B |
| A | R | A | ■ | D | A | U |
| L | ■ | M | B | U | ■ | L |
| I | ■ | K | ■ | ■ | ■ | I |
| O | T | A | N | A | ■ | A |

## TOA TOFAUTI 5




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

LIA, GOA, NZI, BUU, ONANA, LUGHA, INAMA, JIONI, ASUBUHI,IMBISHA

## PAKA RANGI




## CHEKA



Alichokifanya daktari

TOFAUTI ya wazazi wa hapa nchini mtoto wa Tanzania na sehemu zingine wakati anapolala inakuwa kama hivi.

Marekani mtoto anapokwenda kulala huagwa na wazazi wake "usiku mwema mwanagu"

Uingereza wazazi wanamuaga mtoto wao "Pata njozi njema mwanetu"

Hispania anapokwenda kulala wazazi humuaambia "usiku mwema mpendwa wetu"

Tanzania mtoto anapotaka kulala wazazi utawasikia "Kesho umke mapema, hatutaki kusikia umechelewa na hela ya mihogo utaikuta mezani"

**SWALI**

Makaa ya mawe yanapatikana wapi hapa Tanzania?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Je, ni kweli wajane wanajitesa wenyewe?

***KARIBU tena msomaji wangu tujadili pamoja mambo yanayosibu familia zetu kila uchao. Kumbuka hakuna jambo linalotokea pasipo na chanzo. Na chanzo chochote ni lazima kimesababishwa.***

Wiki kadhaa mfululizo tumekuwa tukijadili mambo mbalimbali yakihusiana na wajibu wa mwanamke katika ndoa na zaidi sana jinsi anavyopaswa kuchukuliana na wakwe zake.

Makala ya Jumapili iliyopita nilitaja baadhi ya mambo anayopaswa kufanya mwanaume anapokuwa hai. Hii ikimaanisha usimamizi wa kile atakachokuwa ameacha anapokuwa ametangulia mbele za haki.

Nikasema mwanaume mwenye hekima huhudumia familia yake kwa ajili ya maisha ya hapo baadae, iwe yupo hai au la. Afanye maandalizi ya kuacha urithi kwa familia yake iwe ni yeye ametangulia au mke wake.

Hata hivyo, wajane wengi wamekuwa wakipata misukosuko mingi pale waume zao wanapokuwa hawapo. Nikataja baadhi ya mambo wanayopitia ikiwa ni pamoja na kutengwa na ndugu.

Pia, wanadhalilishwa, wengine hulazimishwa kuolewa na ndugu upande wa mume, hunyang'anywa mali na kuachwa kuhudumia watoto peke yao. Husingiziwa uchawi. Wajane huonekana mzigo.

Mpenzi msomaji, hayo na mengine mengi ndiyo yamekuwa yakiwasibu baadhi ya wajane katika jamii nyingi za kiafrika, ikiwemo nchi yetu.

Wapo wasomaji wazuri kadhaa wa safu hii wametoa maoni yao kuhusu makala ya wiki iliyopita iliyobeba kichwa cha maneno "Anayopaswa kufanya mwanaume anapokuwa hai".

Leo, nimjadili msomaji mmoja aliyetuma ujumbe mfupi kupitia simu ya kiganjani. Akauliza hivi; "dada nimekusoma nimekuelewa. Lakini kwa nini wanawake huwa wanapofiwa na waume zao hunyanyasika?

Akaendelea kusema, "Dhambi wanayo wao wenyewe. Kwa mfano, unaweza kumrithisha mali mkeo. Mume akafariki na baada ya muda katika hiyo nyumba uliyoijenga kwa jasho akamwingiza mwanaume mwingine.

"Je, ni nani ndugu atakayekubali ujinga huo? Hapo ndipo ninaposema dhambi wanayo wao wenyewe. Wanawake wengi ni wajane na huwa wanatutanguliza mapema sana!" anamalizia ujumbe wake Bw. Issa wa Korogwe, Tanga.

Msomaji wangu, bila shaka umempata vema Bw. Issa kwa maoni yake kuhusu mateso kwa wajane. Maoni yake mimi yamenikumbusha mbali wakati nikiwa kazini katika miaka ya 1990, nikiandika habari za maisha katika jamii yetu.

Niliwahi kupewa kazi na Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia watoto(UNICEF), mkoani Kilimanjaro. Nilikuwa nikifuatia miradi ya shirika hilo nchini kuhusu maendeleo ya afya ya mama na mtoto.

Nilipotembelea familia kadhaa eneo fulani, nikagundua kati ya nyumba tano nilizopita, tatu zilikuwa na wajane. Na familia hizi zilionekana kabla zilikuwa na uwezo kiuchumi na watoto walikuwa na elimu nzuri.

Lakini baada ya waume zao kufariki maisha yakabadilika, miradi ikadhulumiwa na ndugu za mume na kuwatenga. Hofu za ndugu eti wakimwachia mali watafurahia na wanaume wengine.

Lakini katika kudadisi, nikapewa siri kwamba wapo baadhi ya wanawake wenye roho ya ukatili, huweka mazingira ya kuhakikisha waume zao wanakufa mapema, hasa baada ya kuwa na mali nyingi ili aweze kuzifurahia akiwa hayupo.

Hawa ni wale wenye roho mbaya na wenye tamaa. Na hawa ndio wale endapo walifanya hivyo kwa kumuondoa mume mapema, huja kuteseka ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa mali zote.

Yupo mama mmoja alikuwa na kazi nzuri ofisi za shirika la kimataifa na mumewe alikuwa na cheo kikubwa serikalini. Lakini mume alipougua na kulazwa hospitali hakutaka hata kwenda kumuona. Aliagiza ndugu zake wakamhudumie.

Hata watoto aliwakataza wasimhudumie baba yao. Hata hivyo mumewe alifariki na alikuwa kinara wa kwanza kufungua mirathi na kugawa mali zote za mume. Leo ni naye ni mgonjwa ndugu wachache tu ndio wanaomjulia hali.

Msomaji wangu, kipo kitu kimoja ambacho watu wengi hawaelewi, kwamba kile alichotengeneza mtu duniani, atakiacha na kutumiwa na wengine. Wakati mwingine hakinufaishi familia yako!

Mungu anasema katika kitabu cha Mhubiri 5:13-15 kwamba, "Kuna balaa mbaya sana niliyoiona chini ya jua, nayo ni hii, mali alizoziweka mwenyewe kwa kujinyima; na mali hizo zimepotea kwa bahati mbaya; naye akiwa amezaa mwana, hamna kitu mkononi mwake".

***Bila shaka lipo jambo umejifunza hapo. Je, una maoni, kisa? Tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581. Tukutane wiki ijayo.***

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi

# Eti tendo la ndoa sasa kwa masharti Uchagani!

MAAJABU ya Musa. Unaambiwa huko Uchagani, hasa maeneo ya Hai, Kirua Vunjo na Kibosho, wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro, sasa hivi ili upewe tendo la ndoa na mke wako, ni lazima utoe pesa ya marejesho ya vikoba!

Si vikoba peke yake. Ipo ile inayoitwa mikopo ya kausha damu, ambayo baadhi ya wanawake ambao wapo kwenye ndoa wamekuwa wakifanya hila kwa kuchukua mikopo hiyo bila kumshirikisha waume zao. Hili sasa ni balaa na wanaume wengi wa Moshi wanalia maana kama huna kipato kumzidi mke au pesa ya maana ya kuhudumia chakula nyumbani, imekula kwako.

Nimewafuatilia wanaokutana na mikasa hii, hasa wanawake wanaosaka pesa kwa nguvu alfajiri hadi jioni. Wanarudi nyumbani, hawajui mume wala watoto mambo yameendaje kutwa nzima. Nilichokibaini ni kuwa bila pesa huna bahati kwa ndugu zetu watafutaji.

Mama yuko 'bize' sokoni asubuhi mpaka jioni. Mfano, leo soko la Kwa Sadala, kesho Memorial, keshokutwa Himo na mtondogoo Tengeru. Ni jambo zuri kujiongeza kama mama na kutafuta maslahi ya kiuchumi kwa ajili yako, watoto wako na mustakabali wa maisha yako ya baadaye, lakini usiingize tamaa mpaka ukaamua kuchukua mkopo umiza ambao utavuruga ndoa yako.

Nimewasikia wanaharakati mbalimbali mkoani Kilimanjaro, wanaofanya kazi na mradi wa majaribio wa utatuzi na usuluhishi wa migogoro ya kifamilia nje ya mahakama na Polisi, unaotumia njia mbadala za utatuzi maarufu kama ADR, wakieleza namna jambo hilo lilivyogeuka pasua kichwa hivi sasa.

Tuna kila sababu ya kulishukuru shirika lisilo la kiserikali la KWIECO, chini ya Wakili mkongwe Elizabeth Minde kwa kuja na mradi huo, ambao umeanza kutekelezwa rasmi katika wilaya zote za mkoa wa Kilimanjaro, ukilenga zaidi kurahisisha upatikanaji wa haki kwa haraka zaidi.

Utekelezaji wa mradi huo wa mwaka mmoja, unaoendeshwa na KWIECO kwa ufadhili wa Shirika la Legal Service Facility Tanzania (LSF), ni mahususi kwa ajili ya uelimishaji jamii husika iliyokumbwa na shauri husika, ambao watashauriwa kuhusiana na sheria zilizoko na taratibu na haki iko upande gani ili wakubaliane na kuridhiana katika kutatua migogoro unaowahusu.

Kwa kuwa tayari mradi huo ulianza Februari, mwaka huu, na utatekelezwa hadi Desemba, ni imani ya Watanzania kwamba wanawake wengi walioangukia katika tatizo hili la ndoa kwa masharti ya kipato, utawapa picha halisi na utawapa mafunzo ya kutosha.

ADR maana yake ni Altenative Disputes Resolution, yaani utatuzi wa migogoro ya kifamilia kwa kutumia njia mbadala, ambazo si za kimahakama wala za kipolisi.

Kwa hiyo mradi huo,utaangalia namna ambavyo utarahisisha upatikanaji wa haki kwa haraka zaidi katika namna ya kuelimisha jamii husika iliyokumbwa na shauri husika.

Mashauri hasa hasa ambayo yataangaliwa zaidi ni mashauri ya ndoa, matunzo kwa watoto, migogoro ya ardhi na mirathi, vipigo na udhalilishaji.

Nimemnukuu Wakili Minde akisema: "Tunayahusisha makundi mbalimbali, ikiwamo wasaidizi wa kisheria walioko Wilaya za Mkoa wa Kilimanjaro, maofisa maendeleo ya jamii, maofisa ustawi wa jamii, dawati la jinsia, wanasheria wa halmashauri na wadau wengine, kulingana na mashauri tutakavyoyaona.

"Wako pia viongozi wa dini na viongozi wa kimila, ambao kwenye mashauri mengi ya kifamilia, hawa ndio wahusika wakuu katika kutatua migogoro hii bila kutumia vyombo vya mamlaka ya kisheria."

Kwa mujibu wa Wakili Minde, mradi huo umeanza kwa kufanya utafiti wa awali, yaani basement survey, ambayo itaendelea kuimarisha muongozo hi wa namna gani wanaweza wakaboresha mradi huo ili kupata mafunzo yatakayowapa mbinu sahihi, ambayo inafaa kutumika kurahisisha upatikanaji au kutatua migogoro ya kifamilia kwa kutumia ADR.

Aidha, Mratibu wa Mradi huo wa KWIECO/ADR, Lilian Mandari, amenukuliwa akisema lengo kuu la mradi huo ni kuchangia utatuzi wa migogoro ya kifamilia kwa kutumia njia mbadala ya utatuzi wa migogoro kwa ufanisi na kupunguza mashauri yanayoweza kutatuliwa kwenye jamii.

Mradi huo utaimarisha maarifa kwa watoa huduma za msaada wa kisheria, kwa kutumia njia mbadala ya utatuzi wa migogoro ya kifamilia, kuongeza uelewa wa jamii kuhusu sheria na kuimarisha mfumo wa kifamilia katika utatuzi wa migogoro kwa kuzingatiwa viwango vya sheria nchini.

Mwanasheria wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Muhusin Kirua, naye amenukuliwa akieleza faida za mradi huo wa KWIECO/ ADR kuwa walengwa wa shauri husika watakaopita katika jopo la watoa huduma, baada ya usuluhishi kufanyika nje ya mahakama kuishi kwa amani na upendo, kwa sababu hakupatikana mshindi katika kesi yao.

Kwamba pamoja na hayo, faida nyingine, huwa ADR inaokoa gharama, kwa sababu unapofungua shauri mahakamani, kuna gharama za ada unatakiwa kulipia lakini kwenye ADR hakuna gharama lakini pia migogoro hiyo itakuwa inasuluhishwa kwa muda mfupi, tofauti na mahakama kesi inaweza ikachukua muda mrefu na faida nyingine ADR inapunguza mlundikano wa kesi mahakamani.


Ukiwasikiliza Polisi, na hasa Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Mrakibu Asia Matauka, anasema: "Katika uwezeshaji wa huu mradi wa kutatua migogoro ya kifamilia kwa njia mbadala, kwa maana ya nje ya mahakama.

"Binafsi ninaona ni mradi mzuri na unaweza kuleta tija katika jamii ukizingatia kwamba sisi ni taasisi ya Jeshi la Polisi kwa ujumla tunashughulikia makosa yote ya jinai, lakini wakati mwingine unakuta tunapokea hizi kesi za migogoro ya kifamilia, migogoro ya ndoa."

Nyie wanawake wa Moshi, hebu acheni aibu! Itakuwaje sasa kama tendo la ndoa litaendelea kutolewa kila mahali, makabila mengine nayo yakaiga mambo yenu ya tendo kwa masharti?

***• Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***

# HARUSI



Watu wengi wamezoea kupiga picha za harusi maeneo ya ufukweni na hoteli za kitalii, lakini mnaweza kufurahia ndoa yenu kwa kwenda maeneo ya kipekee ambayo yatavutia kwa kuwa na kumbukumbu nzuri.

MITINDO







# Jaribu upendeze

UNAPOULIZWA kuhusu mavazi, ni muhimu kutambua ni jinsi gani utakavyoyatumia kwa usahihi kwa ajili ya kukupa furaha na mwonekano mzuri.

Ni muhimu kufahamu upangiliaji wa nguo, wakati unapofikiria unataka kwenda wapi, kufanya nini na unakutana na nani?

Ukishajua hilo, basi unaweza kupangilia vyema nguo utakazovaa ili kuongeza mvuto wa taswira yako.

**SHATI JEUPE**

Shati jeupe linaendana na kila rangi ya nguo. Pale kila kitu kinaposhindikana nyanyua rangi nyeupe, hasa rangi ya nguo ambazo huwa unashindwa jinsi ya kuzipangilia na nguo nyingine.

Unaweza kuivaa na tai ya rangi ya mistari mistari kama unataka kuvaa tai, au unaweza kuvaa pamoja na sweta lenye kola ya V.

**NGUO RANGI HAFIFU**

Rangi ya hafifu inaendana na rangi yeyote ile angavu. Ni rangi nzuri ya kupunguza ukali wa rangi nyingine, kwa hiyo kama unataka kufanya majaribio ya kuvaa rangi yeyote jaribu kuichanganya na rangi ya ugoro na utaona jinsi utakavyotokelezea.

**NGUO ZINAZONG'AA**

Vaa nguo zenye mng'ao zinazoendana ili uweze kutokelezea vyema. Hakikisha thamani ya rangi ziwe zinaendana, nikiongelea thamani ya rangi na maanisha mng'ao wa nguo uwe unaendana.

Kama umevaa suruali rangi hafifu ambayo haing'ai basi na shati lazima vile vile liwe rangi hafifu.

**RANGI ZINAZORANDANA**

Vaa kwa kuendana na rangi zinazoshabiana ili kukupa mwonekano maridadi.

Rangi zinazoshabihiana ni zile zinapingana kwenye duara la rangi, kwa mfano nyekundu na kijani, njano na zambarau, bluu na rangi ya machungwa.

UREMBO



USO WENYE RAHA

# Kicheko kunoga

MENO meupe yenye afya ni ufunguo wa tabasamu zuri, hata kama hautazungumza jambo lakini utaonekana mwenye furaha.

Iwe mwanaume au mwanamke kitu cha kwanza cha kutambulisha muonekano wako ni tabasamu linalotoka kinywani mwako.

Kwa miaka mingi ni kawaida kuona jinsi meno hupoteza urembo wa asili mweupe na kuanza kutia giza kama matokeo ya vitu tofauti.

Lakini kuna njia za kuzuia madoa kuwa na meno meupe, kitu ambacho watu wote wanapenda kuonyesha tabasamu kila siku.

Zipo njia kadhaa za kuzuia madoa hayo kwenye meno meupe ikiwa madoa yametokea bila wewe kujua.

Lakini kabla ya kutibu tatizo ni muhimu kuepuka sababu kadhaa ambazo husababisha madoa ikiwamo kutosafisha kwa mswaki na dawa.

**Tumia Limao kusafisha**

Ikiwa meno yako yanaonekana ya njano kidogo, inaweza kusababisha kubadilika rangi na kuwa meusi kabisa. Hakikisha unachukua hatua za haraka kuyatibu kabla ya kubadilika rangi kabisa na kuwa meusi.

Hatua ya kwanza chukua limao,kamua maji yake weka kwenye chombo kisafi.

Chukua maji ya limao na weka mdomoni na uache kwa muda kidogo.

Baada ya dakika tano chukua mswaki na anza kusafisha taratibu meno yako.

Rudia hivyo mara tatu kwa wiki na utaanza kuona mabadiliko kwenye meno yako.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Namna ya kutengeneza Piza

PIZA ni chakula ambacho kinapendelewa na watu wengi kwa sababu ni nadra kupatikana kutokana na upikaji wake.

**Mahitaji**

Unga wa ngano vikombe vinne, maziwa ya unga vijiko vya supu viwili, mafuta ya mzaituni nusu kikombe, hamira kijiko cha supu, chumvi kiasi, sukari kijiko cha chai kimoja na maji ya dafu vikombe viwili.

Jinsi ya kupika

Changanya vitu vyote katika bakuli na ukande unga. Ufunike na uache uumuke.

**Sosi ya Pizza**

Kitunguu kilichokatwa kidogo kidogo kimoja, kitunguu saumu kilichokatwa chembe tatu,sosi ya HP na vijiko vya supu vitatu.

Sosi ya tomato, vijiko vya supu supu, pilipili manga kijiko cha chai kimoja na oregano kijiko cha chai nusu.

**Namna ya kutengeneza sosi**

Kaanga vitunguu kisha weka kitunguu saumu na vitu vyote iwe sosi.



Epua vitu vya moto vinavyojazwa juu ya pizza, nyanya zilizokatwa vipande vipande, pilipili mboga iliyokatwa na zaituni ikiwa za kijani au nyeusi.

**Namna ya kutayarisha na kupika**

Tengeneza madonge madogo madogo kisha usukume kidogo tu.

Paka sosi juu ya unga, weka kileo upendacho na mwagia vitu vya kujaza juu ya pizza.

Mwagia cheese kisha oka katika oveni kwa muda wa dakika 20 moto kiasi hadi ziive.

Tayari chakula kwa ajili ya kuliwa na familia yako au na marafiki.

MAISHA NI NYUMBA
Na Restuta James

# Matawi ya miti inapogeuzwa holda za taa

WIKI iliyopita nilikueleza namna ambavyo teknolojia imeendelea kuleta mageuzi kwenye nyanja mbalimbali ikiwamo ya mapambo ya ndani.

Leo ninakuletea mageuzi kwenye eneo la mapambo ya ndani kipengele cha taa. Kwenye eneo hili kuna mabadiliko ya matumizi ya vitu asilia kama mawe uliyoyaona kwenye makala ya wiki iliyopita.

Mageuzi hayo hayajaishia kwenye mawe pekee kwani hadi nakshi za magome ya miti zimeingia kwenye samani na vifaa vya umeme.

Taa iliyopo pichani ni moja ya mapambo ambayo yanatumika kama 'holder' za taa.

Mtaalamu wa mapambo ya ndani na vifaa vya umeme, Johnson Ngowi, anasema magome na matawi ya miti yanatumika kutengeneza holder hizo.

Anasema: "Ndio mageuzi yanayoendelea kama unavyoona hii ni holda ya miti, yenyewe ni pambo na wakati huo huo inaleta nuru ndani."

Anasema taa hizo zinapendeza zaidi kwenye kibaraza, ukuta wa koridoni na meza ya kujipambia (dressing table).

Anasema taa hizi zinapendeza zikiwekwa kwenye ukuta wa pembeni na sio juu (kwenye dari).



# Tumia gharama kidogo katika kubadili mwonekano wa nyumba







BAADA ya miaka kadhaa ya kuishi kwenye nyumba, wengi hutamani kubadilisha mwonekano. Mara nyingi wamiliki wengi wa nyumba hupendelea kurekebisha jengo au kununua samani mpya ambazo hutumia gharama kubwa.

Andiko hili la leo ni kukupa mwanga tu namna ya kuboresha maisha ya nyumbani kwako kwa gharama nafuu na ukabaki unafurahia maisha.

Kumbuka kwamba si tu matumizi makubwa pekee ya pesa ambayo yanaweza kubadilisha au kuleta mvuto wa nyumba, bali hata kwa gharama kidogo tu ya pesa hiyo inauwezo wa kuipendezesha.

Kwa mfano matumizi tofauti ya rangi, makaratasi ya ukutani, vitambaa na malighafi zingine zilizotengenezea samani zako, vina nafasi kubwa ya kubadilisha kabisa mwonekano wa nyumba yako na kukupa wa kuvutia zaidi.

Kwa mfano, kupaka rangi upya kabati la luninga, miguu ya kiti au meza, kubadili kitambaa kilichotengenezea viti au sofa, nako kunasaidia kubadilisha mwonekano katika nyumba yako.

Nyingine ni kubadili vitu kidogo kidogo kama vile taa na fimbo za pazia, mapazia yenyewe, zulia, mapambo ya ukutani na mengineyo.

Viko vitu vingi ambavyo unaweza kuvifanyia marekebisho kwa gharama ndogo ndani ya nyumba yako na ukaifurahia tena na usiichoke, kwa mfano kubadili rangi ya ukuta nayo ni mbinu nyingine.


Pia hata kuchagua kubadili kitu kingine unachoona unatakiwa kufanya hivyo. Kama ni foronya unatakiwa kuangalia zile zinazoendana na zilizoko kwa wakati wa sasa.

Kama vitu vyako vya ndani umevitumia kwa miaka mingi na vimepitwa na wakati na ndiyo maana huenda vinakuchosha na kuiona nyumba yako mbaya, usiikatie tamaa kwa sababu inawezekana kuirudisha katika ubora wake.

Kikubwa ni kuwa mbunifu na kuongeza kidogokidogo vionjo vinavyoendana na wakati katika nyumba yako hiyo. Hata kama huna kipato kikubwa inawezekana. Si lazima uweke vyote kwa pamoja lakini kadiri unavyojaliwa, unabadili cha zamani na unaweka kinachoendana na wakati wa sasa. Utanunua pazia leo lakini siku nyingine kitu kingine na hii pia itasaidia nyumba yako kuonekana mpya kila siku.

Ni ukweli kuwa vitu vya nyumbani vinabadilika kila baada ya kipindi fulani, zuria ulilonunua miaka mitano iliyopita, haliwezi kuendana na wakati huu.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
NIPO NJOMBE NIKIRUDI NAKUJA KUKUREKEBISHIA DENI LAKO LOOOTE!
DUH! NILIKUWA NAJIULIZA NIMERITHI WAPI?
TANDALE KWA MFUGA UMBWA
TUACHE NA SISI TUZIANIKE SILAHA ZETU... HATA UKINUNA TUNAZIANIKA KWEUPE
TOKA LINI??? AU NDIO MABADILIKO YA TABIA NCHI AU NDIO ZAMA ZA KIDIJITALI TUYAONE TUSIYOWAHI KUYAONA? 'MIE STAKI!'
KILA NIKIJA KWAKO NAKUTA KISAMVU MCHICHA, MNAVU AU MATEMBELE LAKINI SIO NYAMA
HIYO NI 'TEKNIKI' YA KUISHI NA MKOPO WA 'KAUSHA DAMU' BILA KUTETEREKA KIAFYA
MGANGA TOKA MOSHI KILIMANJARO
DEREVA SPIKA UMENUNUA WAPI?
OYA! USINIVURUGE SUBIRI USHUKE!
UNATAKA KUM-LETEA SABUFA LA MKWEO?
MZAA CHEMA KAFUATA NINI KWENYE STORI ZAKO ZA HOVYO NINGEKUWA MIE NSHAKUBAMIZA BICHWA LAKO!
WACHEZAJI WAO WENGI WANA MATEGE WALA SINA MCHECHETO NAO
UTAAMBULIA KUBEBA VIKOMBE VYA CHAI, LAKINI VYA UBINGWA SAHAU KABISA!
'MBONA POVU?'
ONDOKA BHANA USIJE UKANIFIA UKALITIA DOA JAMBO LETU LEO
JAMBO UTAKUWA NALO WEWE BHANA! KAMA HODARI MTAMBULISHE 'MESI'
DOKTA
NIPO BIZE NATAMBULISHA MITAMBO YA MAANGAMIZI YA LIGI
WE NENG'ENEKA ALAFU UNILISHE USIKU CHAKULA CHA MCHANA UTAONDOKA KWENU NA MIKOFI JUU!
*KINYUNYIZO CHA LEO...
LANGO LA JELA HALIBISHWI HODI...

# MATUKIO KATIKA PICHA



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula (wa pili kulia), akimsikiliza Mhandisi Goodluck Masika (kulia), wakati akikagua maendeleo ya ujenzi wa mradi wa soko la madini ya tanzanite katika mji mdogo wa Mirerani, Simanjiro mkoani Manyara, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**



Mwanafunzi wa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Karibu ya Temeke, Mwajuma Emma, akichangia mada katika mkutano wa kujadili mbinu za kutokomeza ukatili wa kijinsia, ulioandaliwa na shirika la Usawa wa Kijinsia Tanzania (SUKITA) kwa kushirikiana na Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF), shuleni hapo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Mafundi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), wakiunganisha huduma mpya ya maji eneo la njia panda ya Goba Tegeta A, Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Wafanyakazi wa kampuni ya usafi wakizoa taka huku wakiwa hawajavaa vifaa vya kujikinga mikononi, eneo la Mbezi Mwisho, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam juzi, kitendo kinachoweza kuhatarisha usalama wa afya zao. **PICHA: SABATO KASIKA**



Gari dogo likiwa limetumbukia kwenye mtaro wa maji ya mvua, baada ya kugongwa kwa nyuma na lori katika eneo la Tazara, Dar es Salaam hivi karibuni. Hakuna mtu aliyejeruhiwa. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Binti mwenye ualbino, Diana Ngongomi, akiwaelekeza washiriki wenzake jinsi ya kutumia mashine ya kupuliza upepo kusafisha shamba wakati wa mafunzo ya kilimo cha miti na utunzaji miti yanayotolewa na mradi wa Youth Agency Mufindi (YAM), Mufindi mkoani Iringa hivi karibuni. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

SAFU

MAKALA

# KILIMO CHA KISASA KITAZAMWE UPYA



Na Magabilo Masambu

Msisitizo mkubwa ukawa matokeo makubwa bila kutazama zaidi ubora wa matokeo hayo si kwa maana ya ufaulu wake, lakini kwa maana ya maarifa na ujuzi utakaowafanya watu wajiajiri.

TUKIWA katika msimu wa maonyesho ya Nanenane ambao wakulima, wafugaji na wavuvi wanapata nafasi ya kuonyesha bidhaa mbalimbali wanazozizalisha mashambani na viwandani pamoja na kutoa elimu kuhusu kilimo, ufugaji na uvuvi, ni muhimu kuendelea kukumbushana mambo kadhaa hasa yanayogusa afya zetu kama watumiaji wa bidhaa zitokanazo na sekta hizo.

Ni kweli kwamba kila mtu anatamani matokeo makubwa kwa kila jambo analolifanya iwe ni kilimo, ufugaji, uvuvi au lingine lolote. Tumekuwa na tabia ya kupenda wingi bila kujali ubora na usalama.

Tulianza kwenye elimu mtazamo wetu ukawa kupeleka vijana wengi sekondari huku tukidhani kwamba tutakuwa tumetatua changamoto za elimu.

Msisitizo mkubwa ukawa matokeo makubwa bila kutazama zaidi ubora wa matokeo hayo si kwa maana ya ufaulu wake, lakini kwa maana ya maarifa na ujuzi utakaowafanya watu wajiajiri.

Tulifanikiwa na sasa shule zote nchini zinashindana juu ya matokeo ya mitihani si juu ya ujuzi.

Baadaye tukahamia kwenye kilimo. Sina uhakika kama wote tumeona kama ninavyotazama. Awali, tulikuwa na mbegu zetu za asili za mazao, matunda na mboga. Mara tukaambiwa tunatakiwa kuzalisha kwa wingi na kwamba hizi za asili zinafanya tupate mavuno kidogo.

Tukaletewa mbegu tunazoambiwa ni za kisasa na kwamba hizi zinazaa maradufu lakini tukaambiwa hazipandwi hivi hivi, hivyo lazima ziambatane na mambo mengine kama vile mbolea za kupandia, kukuzia lakini pia eti huwezi kuvuna kama hutapiga dawa za kuua wadudu!

Hili la dawa likanikumbusha nyakati zile nilipokuwa kijijini Bulenda Bufwe kwamba zao pekee lililokuwa likipigwa dawa lilikuwa pamba na ile dawa ilikuwa ikitokea pengine ng'ombe au mbuzi akala majani ya pamba muda mfupi baada ya kupuliza, alikuwa anakufa. Sasa nikajiuliza hivi huu utamaduni wa kupuliza dawa katika mazao tunayotumia kama chakula ni kweli umefanyika utafiti wa kutosha na kuleta majibu kwamba dawa hizo hazina athari zozote kwa afya zetu?

Ikanikumbusha zaidi kwamba mbona zamani tulikuwa tukivuna mahindi yetu haya ya kienyeji, tulikuwa tunachagua mahindi ya mbegu tunatundika kwenye mti au jikoni mpaka yanafika msimu wa pili bila kuoza?

Leo ukishamaliza kuvuna mahindi bado unaambiwa weka dawa ili yasiliwe na wadudu, yaani mahindi ambayo wadudu hawali ni salama kwa binadamu.

Lakini nikakumbuka jambo lingine mwaka 1995, babu yangu alikuwa mwenyekiti wa serikali ya kijiji wakati ule Kanda ya ziwa palikuwa na uhalifu wa kutumia sumu kuvua Samaki.

Wale waliokuwa wakikamatwa pamoja na mitumbwi yao walikuwa wakiadhibiwa kwetu ikiwa ni pamoja na kutaifisha mitumbwi na boti zao.

Haya yalifanyika kwa ajili ya kulinda afya za walaji. Sisi walewale tuliopinga walaji kula sumu kwenye Samaki, tumeona ni halali tule sumu kwenye mahindi, kabichi, mboga na matunda! Tutakuwa salama kweli?

Mimi si daktari na siwezi kuthibitisha hili lakini utafiti uendelee kufanyika kubaini chanzo cha ongezeko la wagonjwa wa saratani kwa sababu mwaka 2006 nilipata nafasi ya kutembelea Hospitali ya Ocean Road na wakati huo palikuwa na kitengo cha wagonjwa wa salatani.

Wakati ule wagonjwa walikuwa wachache lakini sijapata nafasi ya kurudi pale siku za hivi karibuni.

Lakini kwa vyovyote vile idadi itakuwa imeongezeka maradufu. Inawezekana saratani hizo zinatokana na sababu mbalimbali, lakini mojawapo yaweza kuwa matumizi ya sumu katika vyakula tunavyotumia kuanzia kwenye wale samaki wenye sumu waliokuwa wakikamatwa wakati ule.

Jambo baya zaidi ni kwamba huku kuhitaji matokeo makubwa sasa kumeharibu kabisa ardhi yetu. Leo huwezi kulima bila kutumia mbolea wala dawa ukavuna.

Ni sehemu chache vijijini zimebaki lakini kwa kweli hali ni mbaya.

Najaribu kuwaza miaka ijayo uzalishaji wetu katika kilimo utakuwaje? Je, ni mpango uliojificha kwenye matokeo makubwa ili baadaye tusizalishe chochote na tutegemee misaada kutoka mahali fulani?

Tusipokuwa makini tutakuwa tegemezi tangu kwenye elimu mpaka kwenye uzalishaji wa chakula chetu wenyewe.

Kweli waungwana tunasomesha wataalamu wetu wa kilimo wanaokwenda kuua mbegu zetu za asili kwa kisingizio cha mavuno mengi? Je, tuna tofauti gani na wale waliokuwa wanatumia sumu kuuwa samaki wengi kwa wakati mmoja lakini madhara yake yakiwa makubwa? Leo samaki wameisha Ziwa Victoria lakini magonjwa kwa watu yanaongezeka.

Serikali inapowekeza nguvu kubwa sana katika kujenga hospitali na vituo vya afya kila kata, juhudi hizo hazitakuwa na maana kama hatutawekeza zaidi katika kukinga watu. Kwa maana nyingine kujenga huduma za afya bila kuzuia visababishi vya magonjwa ni sawa na kukata matawi ya mti huku tukitegemea mti utakauka kumbe mvua ikinyesha matawi yanachipua upya.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Mwanamume aliyetishiwa kifo kusudi amwache mpenzi wake



Na Adam Fungamwango

Baada ya kutamba na kibao cha 'Kila Munu Ave na Kwao' alichokifyatua akiwa na CTU Les Mwenge ya Arusha katikati ya miaka ya 1980, alichukuliwa na mwanasiasa na mfanyabiashara maarufu ambaye alikuwa mpenzi mkubwa wa muziki, Dk. Alex Khalid Mtavala (naye sasa marehemu) kuunda bendi hiyo.

FIKIRIA wewe mwanamume una mpenzi wako mnapendana kwa dhati lakini kwa sababu ni mzuri na mrembo kupita kiasi, anatetemesha wanaume wengine ambao wana uwezo wa kipesa, madaraka na vingine vingine vyenye ushawishi.

Wanaume hao wanamuhitaji mwanamke huyo lakini kikwazo ni wewe, hivyo wanaamua kukufuata na kukupa vitisho ili umwache wamchukue.

Sijui utachukua hatua gani. Katika hili najua kila mmoja anaweza kuwa na uamuzi wake.

Kuna mtu mmoja yalimpata lakini uamuzi wake ulikuwa wa ajabu.

Yeye aliamua kuwaachia ili kunusuru roho yake lakini kitendo hicho alikifanya kwa kutoa maneno ya uchungu sana.

Anampenda msichana lakini watu wenye roho mbaya, wanaomtishia kung'oa roho yake nao wamemsimamia kuangalia nini anafanya.

Anakubali kumwacha ili wamchukue au anakataa wamuue.

Kisa hiki kiko kwenye wimbo uliotoka miaka ya 1990, ukipigwa na bendi ya Makondeko Six Band, mtunzi wake Harila Tongolanga (sasa marehemu).

Baada ya kutamba na kibao cha 'Kila Munu Ave na Kwao' alichokifyatua akiwa na CTU Les Mwenge ya Arusha katikati ya miaka ya 1980, alichukuliwa na mwanasiasa na mfanyabiashara maarufu ambaye alikuwa mpenzi mkubwa wa muziki, Dk. Alex Khalid Mtavala (naye sasa marehemu) kuunda bendi hiyo.

Tongolanga mwenyewe ndiye aliyekuwa kiongozi wa bendi hiyo ambayo ilikuwa na mkusanyiko wa wanamuziki mbalimbali na kutoa vibao mbalimbali vikali kweli kweli, kikiwamo mwendelezo wa nyimbo kama 'Kila Munu Ave na Kwao.'

Moja ya nyimbo zilizorekodiwa ni 'Saidaru', ambao unazungumzia kisa cha mwanamume mwenye hali ya chini kupendana na msichana mrembo hali iliyomweka matatani.

Tuanze kuangalia mashairi ya wimbo huu, jamaa alivyomfuata mpenzi wake na kuanza kumwambia jambo ambalo lilimshangaza hata msichana mwenyewe.

"Hallo Saida mama Munira mwana mama aa, nyota nadhifu wa moyo wangu Saida mama, naomba unikubalie ooo sheri ee, kama nilivyo kukubalia tukawa sote.

Hakika najutia mie mwana mama aa nimejitosa ndani ya moto, kwa matatizo kulikubali ombi lako, oooh sherie ee kwao ni kero kwa wasiopenda niwe na wewe.

"Saida we u mrembo, haikubakishwa, u nadhifu umbile lako, tele kwa tele, uzuri wako na hali yangu ya ufukara kwan ni kero kwa wasiopenda niwe na wewe."

Jamaa anamwambia mpenzi wake kuwa anampenda na ataendelea kumpenda lakini anajuta kulikubali ombi la kuwa wapenzi kwa sababu ni kama sasa yuko ndani ya moto.

Anamsifia mpenzi wake kuwa ni mrembo kwa kile kitu, lakini uzuri alionao na hali yake imekuwa ndiyo fimbo ya kumpigia.

Wanamwambia kuwa yeye hana hadhi ya kuwa na mwanamke mzuri kama yeye na kashfa kibao ambazo zimekuwa zinamuumiza.

"Kitachonitesa rohoni mimi Sai wangu, wanitisha mimi kifo kitanifika, ikiwa sijaridhia ooo sheri eee kuwaachia wewe kipenzi changu."

Kazi ipo hapa. Inawezekana jamaa angeweza kuvumilia kashfa lakini wanaomtaka mwanamke wamemtishia kuwa watamwondoa duniani kama hajamwacha ili wenye nazo wamchukue. Je anachukua hatua gani?

"Ninachokuomba sasa Saida, imenibidi ni bora nijivue eee, hilo pendo, nimewape nafasi wanaomini umeshushwa kwa ajili yao si vema uwe na mimi." Uamuzi mzito na wa uchungu, mwanaume anatangaza kujivua penzi ili kuwapa nafasi ya watu wanaoamini kuwa mwanamke huyo ameshushwa kwa ajili yao kiasi cha kumtishia maisha.

"Ingawa niliapa na wewe, mwana mama aa, tusingetengana nawe mpaka kifo, lakini imetubidi mama tutengane ee, niwaridhishe wale wote wabaya kwenye pendo letu."

Ujumbe mwingine wa uchungu kwa jamaa anayesema ingawa waliapizana kuwa hawatotengena mpaka kifo lakini yeye inabidi watengane ili waridhishe wale wote wabaya kwenye penzi lao wafurahi.

"Nilipokutana nawe mara ya kwanza sheri Saidaru, uliniomba dhamira yako nikukubalie, nilikubali lakini moyo ulishuku jambo, mama aa ningezua mambo, mama aa ningezua mambo mazito.

Nilijitizama mara zote na kujirudia, nijitazama mara zote na kujirudia nikabashiri ipo siku moja mie nitalipata kero, ooo niligundua ipo siku moja mie nitapata kero, na masimango kwa ufukara wangu, ooo na mama kwa ufukara wangu."

Inaonyesha kuwa pamoja na ufukara wake, mwanamke ndiye aliyeonyesha kuanzisha mapenzi hayo.

Tongolanga anasema alikubali lakini moyo wake ulikuwa mzito kuwa huenda baadaye kunaweza kutokea matatizo kutokana na hali yake duni kwa kumpenda msichana mrembo kama yule.

**Una maoni gani katika hili? Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Kafie kwenu-5

CAROLINA, binti mrembo, aliyeumbwa akaumbika, mwenyewe anajiita Carry. Akifahamu fika jinsi alivyo mzuri na kubabaisha kila mwanaume anayekutana naye barabarani, anageuka kuwa mtu mwenye kiburi, jeuri, dharau na majivuno kwa watu. Atamsalimia yule tu aliyempenda kumsalimia. Ataongea na mtu atakayemchagua na si kila mtu. Anaweza kuziba hata pua akipita mtu ambaye yeye anaona si wa hadhi yake. Si mwanaume wala mwanamke. Jirani na anapoishi, kuna kijana mgeni asiyepungua miaka 25 hivi aliyehamia hivi karibu eneo la Kinondoni Moscow. Anaitwa James. Alikuwa kijana anayeishi maisha ya hali ya chini, akipanga chumba kimoja. Jicho lake naye liliona urembo wa Carry. Akaamua kujaribu. Kilichompata hatosahau maishani mwake. Fuatilia hadithi hii ya kusikitisha, kuhuzunisha, kufurahisha, kuburudisha na kufundisha kwa wakati mmoja.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

HIVI wewe baba una wazimu?" Akawa kama amepandishwa tena mashetani kwani alirudia kuongea kwa sauti kubwa na ya hasira tofauti na ile ya dakika chache za mwisho.

"Unampenda nani we masikini? Hivi wewe, au hunioni vizuri, una tatizo la macho? Hebu niangalie kwanza. Unaniona nilivyo." Carry akaanza kugeuka kwa madaha akimuonyesha uzuri aliojaaliwa na mwenyezi Mungu.

"Umeniona eee, haya, umeridhika? Kama umeniona vizuri nadhani akili yako lazima ikuambie kuwa hii siyo taipu yako. Kwamba mbaya, hauvutii..."

"Basi! Usiendelee tena, maana unaendelea kunidhalilisha barabarani, afadhali tungekuwa ndani dada." James alionekana kama kuchoshwa na ukali wa maneno ya Carry.

Maneno hayo yalionekana kumkasirisha Carry. Akacheka kicheko ambacho si halisi. Ni cha hasira.

"Sasa hapa aliyemdhalilisha mwenzake nani? Wewe ndiyo umenidhalilisha kwa kusimama hapa na kikaragosi kama wewe. Narudia tena ukome, usinichoshe, nisikuchoshe, tusichoshane, kwaheri ya kuonana, hebu nipishe mie." Akaondoka Carry kwa hasira na kumsukuma kwa kutumia mwili James.

Pamoja na kwamba mwili wake ulikuwa mwembamba na laini, lakini alifanikiwa kumtingisha James akapepesuka nusu kuanguka.

Mwili wake pamoja na kwamba ni mkakamavu ulikuwa umeshanyong'onyea kwa maneno aliyovurumishiwa na Carry.

*******************************

Mdogo wangu, jana si nimekutana na yule kaka tuliyekutana naye siku ile pale kichochoroni. Si akaanza kuniongelesha maneno ya ajabu. Mara oh! Eti ananipenda, anataka kunioa, hee anioe mimi yule!"

Carry akamwambia mdogo wake wakiwa wamekaa kwenye kizingiti nje ya mlango wa nyumba waliyokuwa wanaishi.

Mazungumzo hayo yalianza mida ya saa 12:00 jioni baada ya kutoka kazini, kuona na kila akiwa amepumzika huku wakipiga stori za hapa na pale.

Catty akamtazama kwa makini dada yake huku akijua kabisa kilichompata kijana wa watu.

"Mh! Dada, basi hapo si kumchamba huko, maana mimi nakujua vizuri tu tabia yako, nakufahamu, yaani kabla hata hujaanza kuniambia nimeanza kumuonea huruma huyo kaka. Haya hebu niambie ulichomjibu!

"Ushaanza hivyo Catty, yaani kabla sijasema unaanza kunihukumu."

"Kwani sikufahamu, hupigiwi tu unacheza..."

"Kama ulikuwepo mdogo wangu, hukuwepo ila malaika wako alikuwepo, nilimnyambua, unajua kumnyambua, sijui kama atarudia tena..."

"Hapana dada, yule mwenyewe unamuona hali yake, anahitaji kusaidiwa, kufarijiwa ili naye ajione kama mtu mwingine, kwa alivyo ukimnyanyapaa anajiona ni mtu asiyefaa kwenye jamii, mara nyingi watu wa aina ile anajisusa na yeye mwenyewe, anaweza kujiua kwa njia yoyote ile, au kubwa, mbaya na hatari kwa jamii, akaanza kudhuru watu kwa kuwaumiza, kuwajeruhi au akawa mwizi kwa sababu anaona watu wamemtenga, akaamua kufanya hivyo kama kulipa kisasi."

Akanyamaza na kumtazama dada yake.

"Niikwambie mdogo wangu, kibaya zaidi anasema eti kwa hali yake ile anaweza kumudu kunitunza, mbona nilichoka! Nilicheka mwenzangu mbavu sina!"

Kwa mara ya kwanza Catty naye akaangua kicheko, halafu kikamalizika kwa kusema. "Kha! Huko tena alifika mbali. "

"Na yule kaka alivyotung'ang'ania, yaani kutuona siku ile, alivyoniona tu kanikumbuka, kaanza kunisemesha eti wewe na ndugu yako niliwaona siku ile leo nimekukumbuka..."

"Dada bahati hiyo!"

"Bahati gani hiyo mdogo wangu mkosi tu, hivyo mwanaume mwenye uwezo wake akikuona umesimama na yule hata kuongea naye tu si anakushusha thamani!"




"Mh! Dada, basi hapo si kumchamba huko, maana mimi nakujua vizuri tu tabia yako, nakufahamu, yaani kabla hata hujaanza kuniambia nimeanza kumuonea huruma huyo kaka. Haya hebu niambie ulichomjibu!

**********************************

Labda kila mmoja wao alikuwa na bahati au mkosi. Kwa sababu walikutana tena wiki moja baada ya siku ile maeneo ya kuelekea Kinondoni Mkwajuni.

Safari hii ilikuwa ni kwenye kichochoro kile ambacho alibahatika kuwaona kwa mara ya kwanza.

Macho ya James na Carry yalikutana tena. Hapa alikuwa peke yake siyo na mdogo wake kama ilivyokuwa siku ile ya kwanza.

Kila mmoja akawa anakumbuka wiki moja iliyopita walipokabiliana kwa maneno. Macho ya kila mmoja yalitafsiri kila kitu.

Ya Carry yalikuwa makali kama kobra, yakionyesha hakutaka kabisa kukutana na mtu aliyeonana naye.

Macho ya James yalibebwa na tamaa ya kutaka kuongea na mtu aliyekutana naye muda huo.

"Hujambo Carry?" Alijibiwa kwa aliyemsalimia kutema mate chini. Halafu masikio yake yakasikia maneno haya kutoka kinywani kwa msichana yule.

"Sijui mikosi gani hii! Hivi wewe huwa unanivizia, au unanifuata nyuma nyuma?"

"Bahati tu hii mama, kuna kitu kipo kati yetu mimi na wewe!" Jibu hilo lilizidi kumkera Carry.

"Nilikwambia siku ile na narudia tena hii mara ya mwisho kuwa siwezi kuwa na mtu kama wewe, koma na laana zako, huu si uchuro wa mchana kweupe..."

"Nikuulize kitu? Akauliza na kabla hajajibiwa akauliza lingine "Kwani mimi nina kasoro gani?"

"Carry akacheka kicheko cha dharau, akamalizia na kusema, "hujioni?"

"Hivi sisi wengine sijui tuna mkosi gani! Yaani badala ya kupata mwanaume wa maana tunafuatwa na majanga kama haya." Akajiambia, halafu akamgeukia James.

"Hivi hujakoma tu!"

"Hebu tulia nikwambie kitu Carry!"

"Umeniitaje? Si nishakukataza wewe! Naona tu unarudiarudia tu. Kama zuri lichukue."

James hakujibu kitu. Akabaki anamuangalia na kuushangaa uzuri wa Carry.

"Enhee nakusikiliza! Si ulisema unataka kuniambia kitu!"

"Ngoja nikwambie kitu, wewe ni mwanamke mrembo sana, naamini ni wanaume wengi wanakupenda na wenye uwezo kuliko mimi..."

"Wenye pesa zao na mali zao, ongezea hilo." Akamkatisha.

"Ni kweli nafahamu hilo."

"Enhee, sasa mbona unajitia uhayawani!"

"Siku zote mapenzi na pesa ni vitu tofauti. Mapenzi yanatakiwa kwanza yaanze halafu pesa inarutubisha, lakini pesa haiwezi kuanzisha mapenzi..."

"Naona siku hizi we bwana umekuwa mtunzi mzuri wa nyimbo, tafuta mfadhili au mdhamini akupeleke studio, utatoka rafiki yangu ili uondokane na hali uliyonayo."

"Narudia vile vile kumwambia Carry kuwa nakupenda."

"Koma wee usiniletee uchuro hapa. Kwanza ishakuwa mkosi, na safari yangu niliyoipanga kwenda siendi tena, naweza kupata majanga makubwa kuliko haya, ngoja nirudi zangu tu nyumbani."

"Poa, kwaheri Carry."

Hakujibiwa.


Akaondoka kwa hasira kurejea nyumbani. Hasira zake hazikuwa moyoni tu, hata alivyokuwa anatembea alionekana hivyo.

Alisahau pozi zake za kutembea kwa madaha kama twiga.

Bado James aliendelea kumtazama hadi akipopotea kwa kukata kona kwenye njia inayoelekea kwao.

**ITAENDELEA JUMAPILI**

## HABARI BURUDANI



# ALI KIBA KULE, DIAMOND KULE

USHINDANI kati ya wasanii wakongwe wa muziki wa Bongo fleva, Diamond Platnumz na Ali Kiba, unazidi kukolea kiasi ambacho mmoja anapokanyaga sehemu moja, mwingine anasikika upande wa pili.

Wasanii hao ambao kwa sasa wapo katika malumbano makali, wamejikuta wakipiganiwa katika klabu pinzani za soka za Yanga na Simba kiasi ambacho kimeleta mvuto wa aina yake.

Ali Kiba atapamba kwa burudani zake katika tamasha la Simba Day leo katika uwanja wa Mkapa, huku akijitambulisha kwamba yeye ni mnyama mpya.

Upande wa pili, Diamond atakwenda na Yanga kuzindua makala maalum kwa ajili ya historia na kutunza kumbukumbu ya vizazi vijavyo.

katika Uzinduzi huo utakaofanyika kesho katika Kumbi ya Century Cinemax uliyopo Dar Free Market jijini Dar es Salaam.

# Zuchu amwaga mboga

MSANII wa muziki wa Bongo fleva, Zuhura Othman maarufu kama Zuchu amemwaga mboga baada ya kuweka hadharani namna wasanii wanavyonunua watu wa kutazama video zao katika mitandao kama YouTube.

Mwimbaji huyo wa kibao kipya cha 'Honey' amedai kuwa wanamuziki wengi hawaziimbi nyimbo ambazo zinaweza kuvuma kama zake, badala yake wanawalipa watu nyimbo hizo kuwa na idadi kubwa ya watazamaji.

Katika ukurasa wake wa Instragram, Zuchu ameeleza" Nawaza sana kama msanii, umejisikiaje kununua viewers (Watazamaji)? Ni kama unakuwa unajua nafasi yako ila ndiyo hivyo tena unaificha ficha kimoyomoyo...unajisikiaje kwani. Ni Tanzania pekee."



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### SILVA ATAKIWA BARCA

BARCELONA itamfanya kiungo wa Manchester City, Bernardo Silva, 28, kipaumbele chao huku winga wa Ufaransa, Ousmane Dembele (26), akitarajiwa kujiunga na Paris St-Germain. ***(Mundo Deportivo)***

### MOYES KITI CHA MOTO

KAZI ya Kocha wa West Ham, David Moyes, iko hatarini huku mvutano ukiongezeka katika klabu hiyo kuhusu malengo yao ya uhamisho. ***(Mail)***

### ALVAREZ KUTUA WEST HAM

KLABU ya West Ham iko tayari kujadili mkataba wa kiungo wa Mexico, Edson Alvarez, 25 na Ajax, baada ya kukubaliana maslahi binafsi na mchezaji huyo. ***(Fabrizio Romano)***

### UNITED, BAYERN VITANI

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag anataka klabu hiyo kumnunua kiungo wa kati wa Real Madrid, Aurelien Tchouameni, 23, ambaye pia analengwa na vigogo wa Ujerumani, Bayern Munich. ***(Sport)***

### AMRABAT ATAJWA UNITED

KIUNGO wa Morocco, Sofyan Amrabat, 26, ameachwa nje ya kikosi cha Fiorentina kwa ajili ya mechi za kirafiki za kujiandaa kwa msimu ujao wikiendi hii huku Manchester United wakionyesha nia ya kumnunua mchezaji huyo. ***(Manchester Evening News)***

### MADRID, CHELSEA ZACHUANA

REAL Madrid inatazamiwa kumenyana na Chelsea katika kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa Juventus na Serbia, Dusan Vlahovic, 23, endapo juhudi zao za kumleta mshambuliaji wa PSG na Ufaransa, Kylian Mbappe (24), zitashindikana. ***(Cadenaser)***

### PARADES KUTUA CHELSEA

CHELSEA inamfuatilia kiungo wa PSG, Leandro Parades, 29, baada ya sintofahamu katika jitihada zao za kumsajili Ecuador, Moises Caicedo (21). ***(Standard)***

### VAN DE VEN ANUKIA SPURS

KLABU ya Tottenham inakaribia kumnunua mlinzi wa Wolfsburg Mholanzi Micky van de Ven, 22, kwa ada ya thamani ya awali ya euro milioni 40 na ikiwezekana kupanda hadi euro milioni 50 pamoja na nyongeza. ***(Sky Sports)***

### WALKER ABAKISHWA CITY

MANCHESTER City imempa mkataba mpya mlinzi wa England, Kyle Walker, 33, kwa nia ya kumbakisha mchezaji huyo katika klabu hiyo huku Bayern Munich wakionyesha nia ya kutaka kumnunua. ***(Athletic)***

### SOMMER KUJIUNGA NA INTER

INTER Milan imekubali ofa ya Bayern Munich kwa mlinda mlango wa Uswisi, Yann Sommer, 34 na mchezaji huyo atafanyiwa vipimo vya matibabu wiki ijayo kabla ya kusaini mkataba wa miaka miwili na klabu hiyo ya Italia. ***(Football Italia)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# BAYERN YATUMA OFA YA MWISHO KWA KANE

**MUNICH,** Ujerumani

**Kiu ya kushinda mataji inamsukuma nyota huyo kuondoka katika...**

BAYERN Munich imeiwekea Tottenham Hotspur ofa mpya na ya mwisho ya zaidi ya euro milioni 100 kwa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya England, Harry Kane, vyanzo vimeiambia ESPN.

> **Vyanzo viliiambia ESPN ofa hiyo mpya ya Bayern Munich imehakikishiwa euro milioni 100 na ongezeko la euro milioni 20.**

Kane mwenye umri wa miaka 30 yuko katika miezi 12 ya mwisho ya mkataba wake na Bayern Munich wako tayari kutumia fedha ya uhamisho wao wa awali zaidi ya euro milioni 80 iliyolipwa kwa Atletico Madrid kumnunua mlinzi, Lucas Hernandez ili kumnasa raia huyo wa England.

Bayern Munich sasa wanasubiri jibu kutoka kwa Spurs na wametishia kusonga mbele katika malengo mengine ikiwa ofa hiyo haitafanikiwa.

Vyanzo viliiambia ESPN Kane hana nia ya kusaini mkataba mpya na Spurs msimu huu wa joto na kuiacha klabu kufanya uamuzi ikiwa itaingiza fedha sasa au hatari ya kupoteza mali yao ya bei bila malipo mwishoni mwa msimu.

Kane amekuwa akilengwa na Bayern Munich msimu wote wa joto lakini kuna nia kwa pande zote kufikia hitimisho haraka iwezekanavyo badala ya kuruhusu hali hiyo kuendelea hadi mwanzoni mwa msimu huu.

Mazungumzo ya ana kwa ana yamefanyika wiki hii kati ya Mwenyekiti wa Tottenham, Daniel Levy na Mtendaji Mkuu wa Bayern, Jan-Christian Dreesen na kuna matumaini Kane yuko tayari kujiunga na mabingwa hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, ikiwa klabu hizo mbili zitakubaliana ada.

Kane amefunga mabao 212 ya Ligi Kuu England na yuko umbali wa kuifikia rekodi ya muda wote ya Alan Shearer (mabao 260) lakini anachochewa na kutaka kushinda taji akiwa hajawahi kunyanyua kombe lolote akiwa na Tottenham au England.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,139,8
MECHI KALI
MANCHESTER CITY
VERSUS
ARSENAL
1 | 1.75
X | 3.68
2 | 3.87
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom | m-pesa
halo pesa
airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# ARSENAL YAJITOSA KUMSAJILI RAYA

**LONDON,** England

ARSENAL imewasilisha ofa ya ufunguzi kwa mlinda mlango wa Brentford, David Raya, kwa mujibu wa 90min.

Brentford imeweka wazi majira yote ya kiangazi iko tayari kumuuza Raya, ambaye yuko katika mwaka wa mwisho, bei yake ya pauni milioni 40 iliwaogopesha Tottenham Hotspur kabla ya kumsajili Guglielmo Vicario badala yake.

Baada ya kuonyesha nia ya kumnunua Raya mapema wiki hii, Arsenal sasa wamefungua ofa ambayo 90min inaeleza inakaribia nusu ya bei ya Brentford.

Pauni milioni 20 za awali zimependekezwa, huku Arsenal pia ikiwa tayari kulipa hadi pauni milioni tano kama nyongeza.

Brentford wanatarajiwa kukataa ofa hiyo huku wakisimama kidete kuhusu bei waliyoiweka.

Kocha, Thomas Frank hivi majuzi alisisitiza kuwa pauni milioni 40 ni nafuu kwa Raya, akiashiria uamuzi wa Arsenal kusajili mchezaji mwingine katika mwaka wa mwisho wa mkataba wao, Declan Rice, kwa pauni milioni 105.

Arsenal haikuwa peke yake katika harakati za kumnasa Raya, huku miamba wa Ujerumani, Bayern Munich pia wakimtaka Mhispania huyo ili kuchukua nafasi ya Yann Sommer, ambaye anatarajiwa kujiunga na Inter Milan.



## 'Maguire kuamua hatima England'

**LONDON,** England

KOCHA Mkuu wa England, Gareth Southgate, amekiri, Harry Maguire, anaweza kujikuta akilazimika kufanya uamuzi juu ya mustakabali wake pale Manchester United, akikiri hawezi kumhakikishia dakika katika timu ya taifa mchezaji ambaye hana namba ya kudumu katika klabu yake.

Southgate amekuwa akimtetea Maguire mara kwa mara na amemwonyesha beki huyo wa kati imani kubwa katika kiwango cha kimataifa, licha ya hana nafasi ya kucheza akiwa na United chini ya Kocha, Erik ten Hag.

Maguire alicheza mechi 31 za klabu msimu uliopita, kati ya hizo nane pekee ndizo alizoanza kwenye Ligi Kuu England na alivuliwa kitambaa cha unahodha wa United msimu uliopita na jukumu hilo amepewa Bruno Fernandes.

Maguire amedhamiria kwa muda mrefu kubaki na kupigania nafasi yake United, ingawa mchezaji huyo amevutiwa na timu kadhaa za Ligi Kuu England.

859,317/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 06/08/23 | 13:00 | Urawa Red Diamonds vs Yokohama Marinos | 2.23 | 3.35 | 2.70 |
| 02. 06/08/23 | 13:00 | Kyoto Sanga FC vs Kashiwa Reysol | 2.22 | 3.05 | 2.90 |
| 03. 06/08/23 | 13:00 | Sagan Tosu vs Avispa Fukuoka | 2.40 | 3.00 | 2.70 |
| 04. 06/08/23 | 13:00 | Thespakusatsu vs Tochigi SC | 2.75 | 2.90 | 2.45 |
| 05. 06/08/23 | 13:00 | Omiya Ardija vs Blaublitz Akita | 2.65 | 2.95 | 2.46 |
| 06. 06/08/23 | 13:00 | Tokushima Vortis vs JEF United Ichihara Chiba | 2.85 | 3.05 | 2.27 |
| 07. 06/08/23 | 14:30 | Karlsruher SC vs Hamburger SV | 2.90 | 3.70 | 2.16 |
| 08. 06/08/23 | 14:30 | 1 FC Nuremberg vs Hannover 96 | 2.16 | 3.55 | 3.00 |
| 09. 06/08/23 | 14:30 | RSC Anderlecht vs Royal Antwerp FC | 2.41 | 3.45 | 2.65 |
| 10. 06/08/23 | 16:00 | Kalmar FF vs AIK | 2.55 | 3.00 | 2.55 |
| 11. 06/08/23 | 16:00 | FK Teplice vs FK Jablonec | 2.60 | 3.20 | 2.37 |
| 12. 06/08/23 | 17:30 | Grasshopper Club Zurich vs FC Basel 1893 | 2.75 | 3.45 | 2.16 |
| 13. 06/08/23 | 18:00 | FK Haugesund vs Rosenborg BK | 2.75 | 3.25 | 2.23 |
| 14. 06/08/23 | 18:00 | Tromsoe IL vs Lillestrom SK | 2.27 | 3.25 | 2.70 |
| 15. 06/08/23 | 18:00 | Blau-Weiss Linz vs TSV Hartberg | 2.39 | 3.25 | 2.55 |
| 16. 06/08/23 | 19:00 | Sunderland AFC vs Ipswich Town | 2.46 | 3.30 | 2.70 |
| 17. 06/08/23 | 20:15 | KV Kortrijk vs St. Truidense VV | 2.80 | 3.40 | 2.33 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 06/08/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2468 | Urawa Red Diamonds vs Yokohama F Marinos | 2.28 | 3.44 | 2.63 |
| 13:00 | 4271 | Roasso Kumamoto vs Mito Hollyhock | 2.17 | 3.18 | 2.98 |
| 14:00 | 4801 | Leicester vs Coventry | 1.51 | 4.06 | 5.55 |
| 14:30 | 3057 | Karlsruher SC vs Hamburger SV | 2.85 | 3.80 | 2.15 |
| 14:30 | 4663 | Nurnberg vs Hannover | 2.26 | 3.49 | 2.84 |
| 14:30 | 5448 | Anderlecht vs Royal Antwerp | 2.47 | 3.42 | 2.58 |
| 14:30 | 5631 | Magdeburg vs Eintracht Braunschweig | 1.96 | 3.54 | 3.49 |
| 16:00 | 2029 | Isloch vs Dinamo Minsk | 7.36 | 4.60 | 1.34 |
| 16:00 | 2584 | Tottenham vs Shakhtar Donetsk | 1.50 | 4.07 | 5.29 |
| 16:00 | 3162 | Kaizer Chiefs vs Chippa Utd | 1.62 | 3.13 | 6.56 |
| 16:00 | 4093 | Kalmar vs AIK Football | 2.87 | 3.08 | 2.29 |
| 16:00 | 4107 | TS Galaxy FC vs Ajax Cape Town | 1.63 | 3.39 | 5.55 |
| 16:30 | 3609 | Leeds vs Cardiff | 1.38 | 4.56 | 6.93 |
| 17:00 | 2957 | Mechelen vs KAA Gent | 3.58 | 3.67 | 1.87 |
| 17:00 | 4428 | Lyngby vs Midtjylland | 3.36 | 3.41 | 2.07 |
| 17:00 | 5172 | Hibernian vs St Mirren | 1.87 | 3.49 | 3.79 |
| 17:30 | 3222 | St. Gallen vs FC Luzern | 1.86 | 3.71 | 3.61 |
| 17:30 | 4614 | Grasshoppers vs FC Basel | 3.21 | 3.52 | 2.04 |
| 18:00 | 1098 | Borussia Dortmund vs Ajax | 1.63 | 3.86 | 4.37 |
| 18:00 | 1241 | Tromso vs Lillestrom | 2.34 | 3.35 | 2.78 |
| 18:00 | 1245 | Ham-Kam vs Brann | 3.66 | 3.82 | 1.82 |
| 18:00 | 2597 | Manchester Utd vs Athletic Bilbao | 1.69 | 3.40 | 4.20 |
| 18:00 | 3149 | RB Salzburg vs WSG Wattens | 1.14 | 7.05 | 11.09 |
| 18:00 | 3663 | Haugesund vs Rosenborg | 2.69 | 3.36 | 2.40 |
| 18:00 | 3790 | Torpedo Zhodino vs Dinamo Brest | 1.79 | 3.46 | 3.97 |
| 18:00 | 4119 | Manchester City vs Arsenal | 1.75 | 3.68 | 3.87 |
| 18:00 | 5021 | Dukla Prague vs Varnsdorf | 1.67 | 3.78 | 4.03 |
| 18:00 | 5357 | Blau Weiss Linz vs TSV Hartberg | 2.24 | 3.28 | 2.78 |
| 18:00 | 5719 | Newcastle vs Villarreal | 2.05 | 3.22 | 3.32 |
| 18:00 | 5799 | Aktobe vs Kairat Almaty | 2.09 | 3.17 | 3.17 |
| 18:00 | 5880 | Sandefjord vs Sarpsborg | 4.32 | 4.12 | 1.64 |
| 18:00 | 5973 | Austria Lustenau vs Austria Vienna | 3.83 | 3.73 | 1.72 |
| 18:30 | 1337 | Cape Town City vs Polokwane City | 1.53 | 3.50 | 6.58 |
| 18:30 | 5762 | NK Mura vs Maribor | 3.59 | 3.48 | 1.84 |
| 19:00 | 1404 | Sunderland vs Ipswich | 2.38 | 3.22 | 2.78 |
| 19:00 | 3350 | Zenit St Petersburg vs Dinamo Moscow | 1.49 | 4.32 | 5.34 |
| 19:00 | 4616 | Nordsjalland vs Brondby | 1.92 | 3.63 | 3.58 |
| 19:00 | 5426 | Slavia Prague vs Zlin | 1.16 | 7.08 | 13.54 |
| 19:00 | 5758 | Dundalk FC vs Shelbourne | 2.35 | 3.03 | 2.82 |
| 19:30 | 5005 | KVC Westerlo vs Brugge | 3.40 | 3.65 | 1.94 |
| 20:00 | 1870 | Shamrock Rovers vs Cork City | 1.43 | 4.04 | 6.06 |
| 20:00 | 4775 | Vojvodina vs Partizan | 2.97 | 3.18 | 2.18 |
| 20:15 | 1029 | Viking vs Bodo Glimt | 2.69 | 3.67 | 2.27 |
| 21:00 | 1595 | Feralpisalo vs Vicenza | 2.38 | 3.22 | 2.91 |
| 21:00 | 4820 | Legia Warszawa vs Ruch Chorzow | 1.33 | 4.54 | 7.26 |
| 21:30 | 3236 | Steaua Bucuresti vs CFR Cluj | 2.11 | 3.24 | 3.24 |
| 21:30 | 5703 | Cesena vs Virtus Entella | 1.95 | 3.44 | 3.70 |
| 22:00 | 2783 | Vasco da Gama vs Gremio | 2.75 | 3.19 | 2.37 |
| 22:00 | 4226 | Sao Paulo vs Atletico Mineiro | 2.10 | 3.14 | 3.28 |
| 22:00 | 5377 | HNK Rijeka vs Istra | 1.60 | 3.68 | 4.64 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



# TANZANIA YAZIOTA FAINALI ZA KOMBE LA DUNIA U-20

**Na Saada Akida**

BAADA ya Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake ya umri chini ya miaka 18 (Tanzania U-18) kutwaa ubingwa wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA U-18), Kocha Mkuu wa timu hiyo, Bakari Shime, amesema sasa nguvu na malengo yake ni kucheza fainali za Kombe la Dunia kwa Wanawake zitakazofanyika mwaka 2027.

**Bao pekee lililoipa Tanzania ubingwa wa mashindano hayo lilifungwa na Winifrida Gerald dakika ya 41 katika mechi iliyokuwa na ushindani dhidi ya Uganda iliyomaliza katika nafasi ya pili.**

Shime alisema kupitia mashindano ya CECAFA U-18, wachezaji wake chipukizi wamepata uzoefu wa mechi za kimataifa na ataendelea na programu mbalimbali kwa ajili ya kuwaendeleza na kuwajenga.

"Hii michuano imekuwa na mwendelezo mzuri kwa timu zetu kwa ajili ya kujiandaa na michuano iliyopo mbele yetu, malengo yetu ni kushiriki mashindano ya Kombe la Dunia ya mwaka 2027, ninaimani tutafanikiwa," alisema Shime.

Naye Rais wa Baraza la Vyama vya Soka Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), Wallace Karia, amesema amefurahishwa na ushindani mkubwa wa soka la wanawake ulioonyeshwa katika mashindano yaliyomalizika Dar es Salaam juzi.

Karia alisema wanachama wa CECAFA wanatakiwa kuendelea kuwalea na kuwalinda wachezaji vijana kwa ajili ya matayarisho ya michezo ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia za mwaka 2027.

Alisema mashindano yalikuwa magumu hadi hatua ya mwisho hakuna nchi ambayo ilikuwa na uhakika wa kutwaa ubingwa kati ya Tanzania na Uganda ambazo zilipata ushindi katika michezo yake mitatu iliyotangulia.

Aliongeza taswira inaonyesha soka la wanawake Tanzania limepiga hatua kubwa na sasa ni tishio katika ukanda huu.

"Hawa wasichana tunatakiwa kuwalea vizuri na kuwatunza kwa sababu ya kuwatayarisha kwa ajili ya michuano ya Kombe la Dunia 2027.

"Kwa timu za Zanzibar, tunafanya jitihada kubwa ya kuhakikisha wanapata mechi nyingi za kirafiki kwa ngazi ya Taifa kwa sababu ya wachezaji wazuri na wenye uwezo wa kusaidia timu katika mashindano hayo ya 2027," alisema Karia.

Aliongeza licha ya timu chache kushiriki, mashindano hayo yamefanikiwa kwa asilimia kubwa.

## Nzegeli, Konkoni watajwa

INATOKA UK. 24

Aliongeza baada ya michezo hiyo miwili ataendelea kuwapa programu maalumu ya mazoezi kwa ajili ya michuano ya Ngao ya Jamii ambayo anaamini itakuwa na changamoto kwa sababu ya matokeo yao ya kufanya vizuri katika msimu uliopita.

Kocha huyo alisema pia anafurahishwa na ushindani wa wachezaji unaoonyesha mazoezini na hii inamsaidia kufahamu uwezo halisi wa kila nyota aliyesajiliwa katika kikosi hicho.

"Matarajio na malengo ya timu yetu ni kufanya vizuri zaidi msimu huu, tunajua kila timu tutakayokutana nayo imejiandaa kufanya vyema, hii ni nzuri kwa sababu inatusaidia kutujenga zaidi, kila mechi kwetu ni kubwa, hatutazembea," Gamondi alisema.



Mashabiki wa Simba Tawi la Shauri Moyo (Mahakama ya Nazi), lililoko katika Wilaya ya Muheza, Tanga wakiwa pamoja baada ya kumaliza kufanya usafi kwenye Kituo cha Afya cha Ubwari kama sehemu ya sherehe za Simba Day 2023 ambazo kilele chake ni leo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## *Ni Simba Day classic*

INATOKA UK. 24

"Hii mechi kwetu ni nzuri kwa sababu tunaenda kujiandaa na mchezo wetu wa Ligi ya Mabingwa Afrika, mchezo huu utanipa mwanga wa kuona mapungufu yetu na kuyafanyia kazi kabla ya kucheza michuano hiyo.

Kuhusu mashabiki wengi kufika uwanjani kwetu ni faida kubwa, ninaimani tunapata uzoefu kwa kuwa tutarejea tena kucheza na Simba baada ya kufanya vizuri katika mchezo wetu wa awali dhidi ya Africa Stars," alisema kocha huyo wa Power Dynamos.

Baada ya mechi hiyo, Simba itaelekea Tanga kwa ajili ya mechi yake ya hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Ngao ya Jamii dhidi ya Singida Fountain Gate itakayochezwa Agosti 10, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani wakati mabingwa watetezi wa taji hilo watakutana na Azam FC kwenye hatua hiyo.

# Michezo

Jumapili Agosti 6, 2023

Nipashe




‘Maguire kuamua hatima England’ UKURASA 22

# Ni Simba Day classic

## ●●● Rais kuwaongoza mashabiki leo huku homa ya ‘Kibegi’ bado...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

RAIS Samia Suluhu Hassan leo anatarajiwa kuwaongoza mashabiki na wanachama wa Wekundu wa Msimbazi katika kuhitimisha kilele cha Tamasha la Simba Day wakati kikosi chake kitakapocheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Power Dynamos kutoka Zambia kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Mbali na mechi hiyo, mashabiki wa Simba watapata nafasi rasmi ya kutambulisha benchi la ufundi na wachezaji wote wa kikosi cha msimu wa 2023/2024, wakiwamo nyota wapya na wanaorejea tena katika timu hiyo.**

Baadhi ya nyota hao ni Aubin Akramo, Willy Onana, Che Fondon Malone pamoja na winga wa zamani wa timu hiyo, Luis Miquissone.

Kutakuwa pia na burudani nyingine mbalimbali, ikiwamo bendi ya muziki wa dansi ya African Stars ‘Twanga Pepeta’, mkali ya bongo fleva, Ali Kiba, Tunda Man, Whozu, Meja Kunta) na Tommy Flavour, wasanii hao wanatarajiwa kuimba nyimbo maalum kuhusu Simba.

Litakuwa ni tamasha la 15 tangu lilipoasisiwa 2009 na aliyekuwa Mwenyekiti wa Klabu hiyo mwaka huu, Hassan Dalali ‘Field Marshal’, ambapo wanachama na mashabiki wa klabu hiyo huanza kwa kufanya kazi na shughuli za kijamii, ikiwamo kutoa misaada katika vituo vya watoto yatima, hospitalini, magereza na kwingineko lakini pia likihusisha zoezi la kutoa damu ili kuwapatia wahitaji.

Katika matamasha 14 ambayo Simba imecheza kabla ya kucheza leo la 15 imeshinda mara nane, sare mbili na kupoteza mechi nne.

Mbali na burudani hizo pia kutakuwa na mechi maalum za timu ya vijana na Simba Queens wakishuka dimbani kucheza mechi ya kirafiki huku nao watakuwa sehemu ya utambulisho lakini pia kutakuwa na mechi maalum kati ya wadhamini wao, Benki ya CRDB dhidi ya NMB.

Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amewataka mashabiki wasiopata tiketi watulie nyumbani na kutotokea uwanjani huku akisema uongozi umeamua mageti ya uwanja huo yatafunguliwa leo kuanzia saa 2:00 ambapo mashabiki watapata burudani kuanza muda huo.

“Wanaokuja kwa Mkapa ni mwenye uhakika wa tiketi, waliochelewa kupata tiketi wasisogee uwanjani kwa sababu usalama ni mzuri na kila sehemu ya uwanja itakuwa na askari kwa ajili ya kuimarisha usalama wa raia,” alisema Ahmed.

Kuelekea mchezo dhidi ya Power Dynamos, Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera ‘Robertinho’ alisema leo ni siku muhimu kwa mashabiki wa timu hiyo na benchi lake la ufundi limejiandaa kukamilisha siku hiyo kwa kuwapa burudani.

Robertinho alisema Power Dynamos ni timu kubwa, anaamini kitakuwa kipimo kizuri kwa wachezaji wake kuelekea katika mashindano yote ya msimu ujao.

“Tunakwenda kuonyesha mchezo mzuri mbele ya mashabiki wetu, wachezaji wako tayari kwa ajili ya mechi hiyo na zilizopo mbele yao, nina matarajio makubwa na nyota wangu baada ya kukaa nao kambini kwa wiki mbili.

Watafanya vizuri, nina kikosi ni bora na chenye ushindani, naweza kuchezesha vikosi viwili na nikapata matokeo kutokana na uwezo wa kila mchezaji,” alisema Robertinho.

Nyota mpya wa timu hiyo, Che Fondoh Malone, alisema anashukuru kuwapo katika sehemu ya wachezaji wa Simba na anawaahidi furaha mashabiki na wanachama wa timu hiyo.

“Ninawafahamu Power Dynamos, ni moja ya timu bora Afrika, tumejiandaa kufanya vizuri katika mechi hiyo, tunakwenda kupambana ili kuhakikisha tunapata matokeo mazuri,” alisema Malone.

Kocha Mkuu wa Power Dynamos, Mwenya Chipepo, alisema anafurahi kuwa sehemu ya sherehe za siku muhimu na timu kubwa ya Simba, anaamini utakuwa mchezo wenye ushindani kwa sababu wanatumia mechi hiyo kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya.

Chipepo alisema watakutana na timu yenye uzoefu wa mashindano ya kimataifa, yenye wachezaji wazuri pamoja na benchi la ufundi na atapata nafasi kubwa ya kuona mapungufu ya kikosi chake kabla ya kuelekea katika mashindano ya kimataifa.

INAENDELEA UK. 23




# Mkongomani Nzegeli, Konkoni watajwa Yanga

**Na Saada Akida**

LICHA ya kupata michezo miwili ya kirafiki dhidi ya timu za hapa nchini, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amefichua bado kikosi chake hakijapata muunganiko mzuri huku akiwataja wachezaji wake wapya akiwamo kiungo, Mkongomani Maxi Nzengeli na Hafiz Konkoni.

Yanga imecheza mechi ya kirafiki dhidi ya Friends Rangers ambayo ilipata ushindi huku ikitoa sare na JKU kutoka Zanzibar, michezo yote imechezwa kwenye uwanja wao wa mazoezi ulioko, Avic Town Kigamboni.

Kikosi cha Yanga kinatarajia kuondoka kesho kuelekea Tanga tayari kwa ajili ya wataanza kutetea taji lao kwa kuvaana na Azam FC, mchezo utakaopigwa Agosti 9, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani.

Akizungumza na Nipashe jana, Gamondi, alisema anahitaji kuona kikosi chake kimeimarika mapema kabla ya kuanza kwa msimu mpya wa ligi na ili kufikia malengo yake, anahitaji kuongeza muda wa kufanya mazoezi.

Gamondi alisema wachezaji wake bado hawajafikia viwango anavyohitaji kuviona na ili kuimarika, atahitaji kuongeza programu maalumu ya mazoezi.

“Sina shida ya uwezo wa wachezaji, kwa sasa nahitaji muda zaidi wa kuendelea kutengeneza muunganiko wa timu hasa kwa upande wa wachezaji wapya, bado hawafikia katika usawa na wale ambao walikuwapo ingawa tunamatarajio makubwa ya kufika mbali, “ alisema Gamondi.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >